bible educational services

# Mwongozo kwa Waalimu

## Wakati na Biblia Daraja la sifuri, la kwanza na la pili

Mfululizo wa C
Somo la kwanza hadi sita

www.besweb.com

## Bible Educational Services

Registered Charity UK (No 1186004)
Imesajiliwa kama shirika la Hisani Uingereza (Namba 1186004)

**Dhamira**
Kuandaa masomo ya Biblia kwa ajili ya wadau ili kutumika kuwakilisha kweli ya Yesu Kristo kwa kizazi kijacho ulimwenguni kote.

**Maono**
Kufikia kizazi kijacho kwa lugha zao kwa kutumia mtaala wetu kamili kwa kukuza na kusaidia mtandao wa kimataifa wa wabia wanaojitolea.

## HABARI KWA UJUMLA

**Bible Educational Services hufanya nini:**

Bible Educational Services (BES) huchapisha masomo ya Biblia ya “Wakati na Biblia/Bibletime”, “Maisha Mapya/New Life” na “Wakusanyaji/Gleaners” kwa Lugha ya Kiingereza na kusaidia vituo vya Shule ya Biblia kwa njia ya Posta pamoja na mashirika mengine ya namna hiyo yanayotumia masomo ya BES huko Uingereza na nchi zingine. BES hufanya hivi kwa kutembelea, kutoa ushauri, kutoa mafunzo na kuunganisha mashirika haya na mengine. Sasa hivi, BES inafanya kazi na vikundi mbalimbali kutoka nchi zingine, vinavyohusika na kutafsiri, kubuni, kuchapisha na kusambaza masomo. Masomo haya yanatolewa bure kabisa kwa kila mtoto.

Kwa mara ya kwanza, masomo ya Wakati na Biblia yalitumika huko Kusini mwa Ireland (Uingereza) zaidi ya miaka sitini iliyopita. Bible Educational Services (BES) wameendelea kuchukua jukumu la uhariri wa masomo ya Wakati na Biblia kwa lugha ya Kiingereza na Lugha zingine. Kwa muda mrefu, Masomo ya Wakati na Biblia (Bibletime) yalichapishwa kwenye muundo wa A4 ambao uliwawezesha wanafunzi kutoka baadhi ya maeneo kutuma masomo yao kwenye kituo cha BES kwa ajili ya kusahihishwa kila baada ya wiki nne. Hivi karibuni, masomo ya miezi sita yamechapishwa kwa muundo wa A5. Muundo huu umefanya utumiaji wa masomo haya uwe rahisi na wa kufaa zaidi kwa makanisa na shule ambazo hazina ufanisi mzuri wa mfumo wa njia ya posta. Tunawashukuru Every Home Crusade au Revival Movement huko Belfast Uingereza kwa kutuwezesha kufanya hivi.

Masomo ya BES ni ya kipekee kwa sababu yameandaliwa ili kutumika nyumbani au kwenye vikundi kama vile kutoka kwenye makanisani na kwenye shule. Masomo haya yameandaliwa kwa kuzingatia vyema mtaala (Syllabus). Masomo yamepangiliwa vizuri na unaomruhusu mwanafunzi kuyatumia hadi atakapotimiza umri wa miaka 20. Masomo yanapatikana katika madaraja matano ambayo yamezingatia umri tofauti. Nayo ni, masomo kwa ajili ya watoto wa chekechea (Daraja 0) ambao wana umri wa chini ya miaka mitano, miaka mitano hadi saba (Daraja la 1), miaka nane hadi kumi (Daraja la Pili), miaka kumi na moja hadi kumi na mitatu (Daraja la Tatu) na miaka kumi na minne hadi kumi na sita (Daraja la Nne). Kuna Mtaala wa miaka mitatu katika kila kikundi cha umri (angalia ukurasa wa 4). Vikundi hivi vya umri vinaweza kutofautiana kulingana na uwezo tofauti wa watoto. Rasilimali na masomo ya Wakati na Biblia yanawapa watoto fursa ya kujifunza Neno la Mungu, kujifunza Habari za Biblia na kujifunza kukabiliana na changamoto zinazotokea maishani mwao kulingana na mwongozo wa Injili ya Bwana Yesu Kristo.

Nakala zilizochapishwa za masomo kwa Lugha ya Kiingereza zinapatikana kwenye tovuti ya BES /BES website – www.besweb.com au kwa katibu ofisi ya BES Uingereza. Yanapatikana pia kwa lugha zingine kwenye tovuti. Kwenye tovuti kuna nyaraka muhimu kwaajili ya mtu yeyote au shirika linalopenda kushirikiana nasi.

## Anuani za mawasiliano za BES

**Ofisi ya Uingereza (Northern Ireland) (Mhifadhi wa masomo yote ya Kiingereza)**
37a Belmore Street, Enniskillen, Northern Ireland BT74 6AA
Simu: +44 286 632 2462

**Katibu wa Uingereza**
Bw. Stephen Gillham,
Barua pepe: stephen.gillham@besweb.com

Tovuti: www.besweb.com
Barua pepe: info@besweb.com

**Mshirika Tanzania (Tanzania Partner)**
World Vision Tanzania
S.L.P. 6070 Arusha, Tanzania
Barua Pepe ya Mawasiliano: david_ombeni@wvi.org
Simu: +255 687 231 757

## MWONGOZO kwa WAALIMU

Mwanzoni, masomo ya Wakati na Biblia yaliandaliwa ili yatumike kwa njia ya posta kukiwepo na kituo cha Shule ya Biblia kwa njia ya posta. Sasa hivi, masomo yanaendelea kutumika kwa wingi hata kwenye sehemu ambazo hazina ufanisi wa kutumia mfumo wa posta au hakuna kabisa mfumo wa posta hasa katika makanisa na shule zilizopo Afrika, India na maeneo mengine. Mwongozo kwa Walimu umeandaliwa kwa wale wanaotumia masomo ya Wakati na Biblia katika hali kama hizo. Mwongozo kwa Walimu katika kitabu hiki umeandaliwa kutumika kwa masomo ya Daraja 0, Daraja la kwanza na Daraja la pili kwa watoto wenye umri kutoka chekechea hadi wastani miaka 10. Masomo ya Daraja 0 hayajajapishwa ila yanaweza kupakuliwa bure kwenye tovuti ya BES.

Kila Mwongozo wa kufundisha hufuata vifungu vile vile vya Biblia vilivyopo katika somo la Wakati na Biblia. Masomo ya Wakati na Biblia na Mwongozo vimeandaliwa vitumike kila wiki. Masomo ya mwezi Aprili yanahusu Pasaka na masomo ya mwezi Desemba yanahusu Krismasi.

Baadhi ya sehemu watakuwa wanatumia masomo yaliyo katika toleo la A4 la kila wiki na wengine watakuwa wanatumia kitabu cha A5 chenye masomo 24 ndani yake. Kwa kawaida, mwalimu au kiongozi hutoa somo la mwezi toleo la A4 na kila wiki sehemu ya kazi hujazwa kanisani au shuleni au hupelekwa nyumbani na kurejeshwa wiki inayofuatia. Mwishoni mwa mwezi, mwalimu au kiongozi hukusanya somo na kwenda kusahihisha kama inavyotakiwa na kumrudishia mwanafunzi/mtoto kazi iliyosahihishwa mapema iwezekanavyo.

Unapotumia kitabu, mwisho wa kila kipindi, vitabu hukusanywa na kusahihishwa. Tumegundua katika sehemu nyingi kuwa, hili haliwezekani. Hivyo basi, pale darasani masomo yanaweza kugawanywa kwa wanafunzi wengine na mwalimu au kiongozi ataongoza usahihishaji wa somo na wanafunzi watasahihisha masomo ya rafiki zao na kutoa maksi. Nyuma ya kitabu kuna sehemu kwa ajili ya kuweka maksi ya kila somo la mwezi na pia mahali pa maoni kuhusu maendeleo ya mwanafunzi. Pia kuna cheti ambacho mwanafunzi anaweza kupewa kinachoonesha asilimia ya alama ambazo mwanafunzi amepata kwa masomo ya miezi sita.

## MAANDALIZI KWA WAALIMU

Mwongozo huu wa Walimu siyu shinikizo ambao hauwapi walimu fursa ya kufanya mambo kwa njia zao wenyewe kulingana na mawazo na mipango yao wenyewe. Haya ni mapendekezo yanayoweza kutumika kwenye utumiaji wa masomo ya Wakati na Biblia.

- **Elewa habari vizuri** – Walimu wanapaswa kuelewa habari ya Biblia vizuri kwa kadiri iwezekanavyo na vile vile somo la Wakati na Biblia linaloendana na habari hiyo ya Biblia. Ni jambo zuri kwa mwalimu kukamilisha somo la Wakati na Biblia kabla ya kipindi. Mwongozo wa kila somo unapaswa kutumiwa kwa umakini kama chombo cha kumsaidia mwalimu anapojiandaa kwa ajili ya somo.
- **Elewa funzo ambalo watoto wanastahili kupata au kujifunza** – Juu ya kila mpangilio wa somo utaona maneno ‘Tunajifunza kuwa’ ikifuatiwa na makusudio mawili ya kujifunza ambayo tunatumaini kwamba watoto watayaelewa baada ya kumsikiliza mwalimu akifundisha na kukamilisha somo la Wakati na Biblia. Kusudio la kwanza la kujifunza jambo linahusu ufahamu wa habari na la pili linamtia moyo mtoto kufikiri juu ya ufahamu huo, kuutumia na kuuitikia. Makusudio haya ya kujifunza ni sentensi kamilifu na fupi ya mawazo au kweli kuu zinazofundishwa katika somo. Walimu wanaweza kuzitumia kwa ajili ya tathimini zao binafsi za ufundishaji na mafunzo ambayo watoto wamepata.
- **Toa Utangulizi** – Kwa masomo yote, tunaanzia mahali ambapo watoto wapo katika uzoefu wao wa hali husika. Tumependekeza njia kadhaa ambazo zinaweza kutumika kufanya utangulizi wa habari ili kuwawezesha watoto kuhusika katika kujadili mwanzo wa habari.
- **Fundisha** – Tumetoa dondoo muhimu katika habari. Tunaamini kwamba walimu hawatazinukuu wakati wanafundisha habari lakini watakuwa na uelewa mzuri wa habari na wataweza kuifundisha katika njia inayofurahisha na kusisimua. Mwalimu atahitaji watoto waelewe mafunzo muhimu kutoka kwenye habari na kuwasaidia kuuelewa mwitikio watakaoupata kutoka kwenye habari waliyojifunza. Kwa usahihi, tumejaribu kuweka pamoja baadhi ya maelezo kwa ajili ya kufundisha habari. Haya yameandikwa katika maandishi *YA MCHALAZO (Italics)*.
- **Jifunze** – Kuna Mstari Muhimu ambao umewekwa katika kila habari. Katika baadhi ya maeneo, kuna Mistari Muhimu miwili. Mstari huu ulioongezwa unaweza kuwa rahisi kwa watoto kujifunza. Tunatumaini kwamba, watoto watajifunza Mistari muhimu na watakumbushiwa mstari huo mara nyingi iwezekanavyo ili waanze kujenga ufahamu wa Mistari muhimu ya Biblia.

- **Kamilisha** – Katika mazingira ya shule, utatambua uwezo wa watoto kwenye kukamilisha kazi na kiasi cha usaidizi ambao wanauhitaji kutoka kwa mwalimu. Kwa baadhi yao, itahitajika mwalimu asome maandishi katika somo na watoto kufuatilia habari ambayo sasa watakuwa wanaielewa. Watoto wengine wanaweza kusoma maandishi ya somo peke yao. Kwa hali yoyote kati ya zilizotajwa, ni wazo zuri kuwahamasisha watoto wawe makini na kuwapa maelekezo muhimu yanayohusiana na maswali. Kama unatumia masomo ya Wakati na Biblia katika maeneo ambayo siyo shule, ni muhimu walimu kuwepo na kuwasaidia watoto ili wasichukulie masomo haya kama kazi isiyo na mvuto au kama mtihani. Masomo haya yanapaswa kuwa ya kufurahisha na kutia moyo. Ni muhimu kuwasifia watoto wanapoendelea kufanya masomo na kujibu maswali.
- **Kumbuka** – Tunashauri matumizi ya maswali mafupi na maigizo ili kuwasaidia watoto kujifunza na kurudia habari ili kuielewa vyema.
- **Kuonesha** – Tunatambua kuwa katika baadhi ya mazingira, sio rahisi kupata vielelezo au video. Lakini, ni muhimu kadiri iwezekanavyo kuwa na picha au vitu vinavyoweza kuwasaidia watoto kuielewa habari vizuri zaidi. Vielelezo vitakuwa muhimu sana wakati ambapo mwalimu anaelezea habari. Kadiri iwezekanavyo kwenye kila somo, tumetoa maelezo kuhusu picha kutoka kwa picha za www.freebibleimages.org (FBI) ambazo zinaweza kupakuliwa bure kwenye tovuti yao. Mwisho wa Mwongozo wa Walimu kuna viambatisho vyenye viungo (hyperlinks) vya picha tofauti na zinazofaa kwa kila habari kutoka kwenye tovuti ya Free Bible Images. Kama kuna kinakilishi (photocopier), baadhi ya picha za Bibletime zinaweza kufanywa kuwa kubwa, kupakwa rangi na kutumiwa kufundisha.

## Kupangilia Muda

- **Ratiba –** Tumeweka ratiba sawa kwenye mwongozo wa kufundisha kila somo lakini mwalimu anaruhusiwa kubadilisha ratiba hii mara kwa mara kulingana na mahitaji ya darasa lake/ watoto anaowafundisha.
    1. Utangulizi na kuwaambia watoto habari husika – Takriban dakika 15
    2. Kufundisha Mstari muhimu – dakika 5 hadi10
    3. Kujaza nakala ya somo – dakika 20
    4. Maswali na shughuli zinginezo- dakika 5 hadi10

Kumbuka msemo muhimu:

“Niambie na nitasahau,
Nioneshe na nitakumbuka,
Nihusishe na nitaelewa”

## Mtaala wa Wakati na Biblia

| | Daraja 0 (Chekechea/Chini ya miaka mitano) Daraja la Kwanza (Miaka mitano hadi saba) Daraja la Pili (Miaka nane hadi kumi) | Daraja la Tatu (Miaka kumi na mmoja hadi kumi na mitatu) | Daraja la Nne (Miaka kumi na minne na zaidi) |
|---|---|---|---|
| SOMO LA KUANZIA | Somo la kuanzia – Utangulizi (Inaandaliwa) | Somo la kuanzia – Utangulizi (Inaandaliwa) | Somo la kuanzia – Utangulizi (Inaandaliwa) |
| MFULULIZO WA A | 1. Mwanzo<br>2. Nuhu<br>3. Petro<br>4. Petro- Msalaba<br>5. Ibrahimu<br>6. Ibrahimu<br>7. Petro<br>8. Petro<br>9. Yakobo<br>10. Wakristo wa Kwanza<br>11. Paulo<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mwanzo<br>2. Nuhu<br>3. Petro<br>4. Petro- Msalaba<br>5. Petro<br>6. Ibrahimu<br>7. Yakobo<br>8. Maombi<br>9. Paulo<br>10. Paulo<br>11. Paulo<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mwanzo na Kuanguka<br>2. Matukio ya Kwanza-Mwanzo<br>3. Petro<br>4. Petro- Msalaba<br>5. Petro<br>6. Ibrahimu<br>7. Yakobo<br>8. Maisha ya Ukristo<br>9. Paulo<br>10. Paulo<br>11. Paulo<br>12. Habari ya Krismasi |
| MFULULIZO WA B | 1. Maisha ya kwanza ya Kristo<br>2. Miujiza<br>3. Bethania<br>4. Msalaba<br>5. Mifano<br>6. Yusufu<br>7. Yusufu<br>8. Watu ambao Yesu alikutana nao<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Musa<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mifano<br>2. Miujiza<br>3. Bethania<br>4. Msalaba<br>5. Wakristo wa kwanza<br>6. Yusufu<br>7. Yusufu<br>8. Walioandika vitabu vya Injili<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Musa<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mifano<br>2. Miujiza<br>3. Bethania<br>4. Msalaba<br>5. Wakristo wa kwanza<br>6. Yakobo na familia yake<br>7. Yusufu<br>8. Matendo ya Mitume 2: 42 – Njia iliyoko mbele<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Amri<br>12. Habari ya Krismasi |
| MFULULIZO WA C | 1. Danieli<br>2. Miujiza zaidi<br>3. Watu ambao Yesu alikutana nao<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruthu na Samweli<br>6. Daudi<br>7. Daudi<br>8. Yoshua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Yona<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Danieli<br>2. Watu ambao Yesu alikutana nao<br>3. Miujiza zaidi<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruthu<br>6. Samweli<br>7. Daudi<br>8 Yoshua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Watu ambao Mungu aliwatumia – Agano la Kale<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Danieli<br>2. Maneno ya Kristo<br>3. Nguvu za Bwana<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruthu<br>6. Samweli<br>7. Daudi<br>8. Yoshua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Watu zaidi wa Agano la Kale<br>12. Habari ya Krismasi |

**C1 Habari ya Kwanza**

**Danieli – Nchi ya ugenini – Habari hii inahusu kumpendeza Mungu kwa kusema 'hapana' kwa yaliyo mabaya.**

**Tunajifunza kuwa:**
- Mungu alimbariki Danieli na rafiki zake kwa sababu walikuwa waaminifu kwake.
- Tunapaswa kuwa waaminifu kwa Mungu hata mambo yanapokuwa magumu.

**Mstari Muhimu:** ***Danieli 1: 20***
**Habari kwenye Biblia:** ***Danieli 1: 1-21***

**TOA UTANGULIZI**

Darasa la Becky lilikuwa likifanya mtihani. Maswali yalikuwa magumu. Mwalimu alikuwa amewahamisha watoto wote kwenye viti ambavyo hawangeweza kuona majibu ya watoto wengine. Lakini Becky bado aliweza kuona majibu aliyokuwa Megan anayajaza. Megan kila wakati alikuwa akiifanya kazi yake vizuri. Becky alifikiri kwa mara hiyo moja tu angeweza kunakili majibu na mwalimu wake hangeweza kujua. Angeweza kupata alama bora katika mtihani na mama yake angefurahi. Lakini je, Mungu angefurahi? Becky alijua ilikuwa muhimu zaidi kutoiba majibu ya mtu mwingine. Alikumbuka kwamba mojawapo ya sheria za Mungu ilisema tusiibe. Kwa hiyo badala ya kudanganya, Becky alifikiri sana kwa makini kuhusu maswali magumu. Baadaye, Becky aligundua kuwa ameyapata vizuri. Kufanya jambo sahihi ilikuwa bora zaidi! Katika somo la leo la Biblia, Danieli na marafiki zake walipaswa kuchagua kati ya kufanya jambo sahihi linalompendeza Mungu au kufanya jambo ambalo lingewarahisishia maisha.

**FUNDISHA**

- Danieli na marafiki zake watatu walikuwa Waebrania (watu waliochaguliwa na Mungu) na waliishi Yerusalemu. Siku moja adui mfalme aliyeitwa Nebukadneza alivamia jiji lao na kuwateka pamoja na watu wengine. Walipelekwa mbali sana huko Babeli ambako walienda katika shule maalumu na kujifunza lugha mpya na pia kuhusu nchi yao mpya. *Waulize watoto kufikiria jambo hili lingekuwaje kwao kama lingewapata.* ***(Daniel 1: 1-4)***
- Danieli na marafiki zake walipewa majina mapya ya Babeli *(angalia majina hayo katika Daraja la Pili)* na kupewa chakula kutoka kwenye meza ya mfalme. Alitaka wawe na nguvu ili wamtumikie katika jumba lake la kifalme. Mfalme Nebukadneza alitaka Danieli na marafiki zake wasahau yote kuhusu nchi yao na Mungu mmoja wa kweli ambaye walimtumikia. ***(Daniel 1: 5-7)***
- *Jadili kwa nini jambo hilo halikuwa zuri.*
- Danieli na rafiki zake walimpenda Mungu na walitaka kumtii ingawa walikuwa katika nchi ya ugenini ambako watu walifuata miungu mingine. Walijua kwamba hawakupaswa kula chakula cha mfalme kwa sababu kilikuwa kimetolewa kwa miungu ya uwongo. *Wangepaswa kufanya nini?* Waliamua kwamba hawatakula chakula cha mfalme ingawa jambo hilo lingeweza kumkasirisha. *Daima tunapaswa kufanya yale ambayo Mungu anasema hata inapoonekana kuwa ni vigumu na watu wengine wanapotaka tufanye jambo jingine tofauti.*
- Walipowaambia wasaidizi wa mfalme kile walichopanga kufanya, wasaidizi hao walikuwa na wasiwasi!
- Ingekuaje kama Danieli na marafiki zake wasingeonekana kuwa na nguvu na afya nzuri kama wale vijana wengine katika shule ya mfalme? ***(Danieli 1: 8-10)*** Danieli aliamini kwamba Mungu atawapa afya njema.
- Aliwaomba wasaidizi wa mfalme wawape mtama na maji tu kwa siku kumi. Wakati ulipokwisha, wasaidizi wa mfalme walishangaa kuona Danieli na rafiki zake wakiwa na afya njema na nguvu kuliko wale watu waliokula chakula cha mfalme. ***(Danieli 1: 11-15)*** *Unafikiri kwanini ilikuwa hivyo?*
- Tangu wakati huo Danieli na rafiki zake walipewa mtama na maji tu. Mungu alikuwa pamoja na Danieli na marafiki zake na akawabariki kwa uaminifu wao kwake. Aliwapa hekima na kumsaidia Danieli kueleza ndoto. ***(Daniel 1: 16-17)*** *Elezea kuwa Danieli na marafiki zake hawakuwa na lishe bora tu, bali pia Mungu alikuwa pamoja nao.*
- Baada ya miaka hiyo mitatu, vijana wote wakaletwa kwa mfalme. Miongoni mwa watu wote mfalme aligundua Danieli na marafiki zake watatu ni bora zaidi. Aliwaona kuwa bora mara kumi zaidi ya washauri aliokuwa nao. *Kazia kwamba walimtanguliza Mungu licha ya uwezekano wa kuadhibiwa kwa kutomtii mfalme.* ***(Danieli 1: 18-21)***
- *Wakristo wanaamini kwamba ni muhimu kusema 'ndiyo' katika mambo yanayompendeza Mungu na kuwa waaminifu Kwake.*

**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**
**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Danieli: Nchi ya ugenini.

**JIFUNZE**

Kama inafaa, fundisha na kuelezea Mstari Muhimu ambao ni sehemu ya habari – ***Danieli 1: 20***.
Daraja la Kwanza watoto wangeweza kujifunza nusu ya pili ya mstari.

**KUMBUKA**

**Daraja la Kwanza** - Darasa linaweza kutengeneza kolagi ya mboga za majani zenye ubora na kuunganishwa na mtaala wa Kula kwa Kuzingatia Afya. Tumia karatasi ya rangi, karatasi ya tishu, kitambaa nk.
**Daraja la Pili** - Wakifanya kazi katika vikundi, watoto wanaweza kujaribu kuigiza hadithi. Amua ni wahusika gani wanahitajika na saidia kuwapanga.

## C1 Habari ya Pili

**Sanamu ya Nebukadneza – Habari hii inahusu marafiki wa Danieli wakisema 'hapana' kwa kile ambacho si sahihi.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Shadraka, Meshaki na Abednego walimwamini na kumtii Mungu.<br>• Tunaweza kumwamini Mungu kuwa pamoja nasi katika jaribu lolote.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Danieli 3: 17***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Danieli 2: 48, 49 na 3: 1-30*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Nebukadneza hakuamini katika kumwabudu Mungu mmoja, wa kweli. Aliabudu sanamu au miungu iliyotengenezwa kwa chuma au mawe, lakini haikuwa na thamani yoyote kwa sababu haikuweza kusaidia mtu yeyote. Danieli na marafiki zake watatu walijua ni kosa kuabudu sanamu kwa sababu Mungu aliamuru hivyo katika amri ya pili – ***Kutoka 20: 4*** |
| **FUNDISHA** | • Marafiki watatu wa Danieli, Shadraka, Meshaki, na Abednego walikuwa wanaume wa Kiebrania waliomwamini Mungu mmoja, wa kweli na walitaka kumtii. *(Wakumbushe watoto matukio katika Habari ya Kwanza)*. Hawangeabudu masanamu. Mungu alikuwa amewasaidia kuwa watu muhimu sana huko Babeli. ***(Danieli 2: 48-49)***<br>• Mfalme Nebukadneza alitengeneza sanamu ya dhahabu. Ilikuwa na urefu wa futi tisini na upana wa futi tisa. (Sawa na takriban magari 24 kila moja likiwa juu ya mwenzake.) Aliamuru watu wote muhimu katika ufalme wake, pamoja na Shadraka, Meshaki, na Abednego waje kwenye sherehe ya pekee. Mfalme aliamuru kwamba wakati wanamuziki wakipiga ala zao, kila mtu anapaswa kuinama na kuabudu sanamu ya dhahabu. Yeyote ambaye hangeinama angetupwa katika tanuru ya moto. *Elezea tanuru ni nini.* ***(Danieli 3: 1-6)***<br>• Muziki ulipopigwa, watu waliinama chini na kuabudu sanamu hiyo. Wote waliinama isipokuwa Shadraka, Meshaki, na Abednego. *Kwa nini hawakufanya hivyo? Walijua Neno la Mungu na kuwa alikuwa ameamuru kwamba watu wake wasisujudie sanamu.* Shadraka, Meshaki, na Abednego hawangemwasi Mungu hata kama ingemaanisha kutupwa katika tanuru ya moto. ***(Danieli 3: 7)***<br>• Baadhi ya washauri wa mfalme walimwambia kwamba Shadraka, Meshaki na Abednego hawakuinamia sanamu yake. Alikasirika! Aliwaambia lazima wasujudu na kuabudu sanamu yake, au angeamuru watupwe ndani ya tanuru. Aliwaambia kwamba hakuna mungu ambaye angekuwa na nguvu za kutosha kuwaokoa. ***(Danieli 3: 8-15)****. Waulize watoto ni nani wanafikiri angekuwa na nguvu za kutosha kuwaokoa watu hao.*<br>• Watu hao watatu wakajibu wakisema, 'Tukitupwa ndani ya tanuru, Mungu wetu tunayemtumikia aweza kutuokoa' *(Mstari Muhimu)*. Mfalme Nebukadneza aliamuru tanuru iwashwe mara saba zaidi. Watu hao watatu walitupwa katika tanuru ya moto. ***(Danieli 3: 16-23)***<br>• Kisha mfalme akaruka juu kwa mshangao. Alikuwa ameamuru watu watatu watupwe ndani ya tanuru, lakini aliweza kuona wanne! Walikuwa wakizunguka kwenye moto bila kujeruhiwa kabisa. Alifikiri mtu wa nne anafanana na, 'mwana wa miungu. ***(Danieli 3: 24-25)***<br>• Mfalme Nebukadneza aliwaamuru kutoka nje ya moto. Wanaume hao hawakudhurika kwa njia yoyote ile. Nebukadneza alimsifu Mungu, akisema kwamba alikuwa amewaokoa kwa sababu walikuwa wamemwamini na kumtii. Alijua kwamba hakuna mungu mwingine ambaye angeweza kuwaokoa watu wake kwa njia hii. Aliwapa wote watatu nyadhifa za juu katika ufalme wake. ***(Danieli 3: 26-30)***<br>• *Elezea kuwa Mungu anataka tumtii na kumwamini kikamilifu. Hii ina maana kwamba tutahitaji kujua Neno la Mungu na kuelewa amri Zake. Ameahidi kuwa atakuwa nasi daima hata katika nyakati za hatari. Ana uwezo wa kutuokoa!* ***Soma Isaya 43: 2***<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Sanamu ya Nebukadneza. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na kuelezea Mstari Muhimu ambao ni sehemu ya habari – ***Danieli 3: 17***.<br>- zingatia kwenye - "Mungu wetu tunayemtumikia aweza kutuokoa". |
| **KUMBUKA** | Tumia maswali haya kwa ajili ya jaribio:<br>• Je! Watu watatu katika habari hii walipewa majina gani?<br>• Mfalme aliitwa nani?<br>• Mfalme Nebukadneza alitengeneza nini?<br>• Tunajuaje kwamba Mungu alichukizwa sana na sanamu hiyo?<br>• Nini kingetokea kwa watu ambao hawangeinamia sanamu?<br>• Watu hao watatu walichagua kumtii Mungu. Je, 'kutii' maana yake nini?<br>• Mfalme alifanya nini alipoona wamelindwa wakawa salama? |

## C1 Habari ya Tatu

**Danieli – Dirisha lililofunguliwa – Habari hii inahusu uaminifu wa Danieli na jinsi alivyoomba kwa Mungu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Wivu wa maadui wa Danieli haukuwa sahihi.<br>• Ikiwa tunampenda Bwana kama Danieli, tutakuwa waaminifu na wa kuaminika.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Danieli 6: 16***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Danieli 6: 1-16*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Daraja la Kwanza- Zungumza kuhusu kelele zinazotolewa na wanyama mbalimbali. Cheza mchezo ambao mtoto hupiga kelele kama mnyama fulani, na wengine wanakisia ni mnyama gani. Hatimaye, kazia kwenye kelele ya simba. Waambie watoto wajaribu kutoa mngurumo mkubwa kisha waambie kwamba simba katika habari ya leo wanasikika hivi, 'Huuu!!!<br>Daraja la Pili - Zungumza kuhusu wivu. Umewahi kuwa na wivu kwa sababu mtu mwingine alichaguliwa kwa kitu fulani, na wewe ukaachwa? Labda hisia hizo zilikuwa na nguvu sana kiasi kwamba ulitamani jambo baya lingempata mtu huyo. Ndivyo ilivyotokea katika habari ya leo. Elezea kuwa wivu ni dhambi na hupelekea chuki. |
| **FUNDISHA** | • Babeli ilikuwa na mfalme mpya aliyeitwa Dario. Kulikuwa na wakubwa watatu huko Babeli na Danieli alikuwa mmoja wao! Daniel alifanya kazi kwa bidii na alifanya kazi yake vizuri sana. Mfalme Dario alitaka kumweka juu ya wakubwa wengine. ***(Danieli 6: 1-3)***<br>• Wale watu wengine waliposikia hayo, walimwonea wivu Danieli. Hawakutaka atawale juu yao Walijaribu kufikiria mambo fulani ya kumwambia mfalme ambayo yangeweza kumfanya asimpende Danieli na kubadili mawazo yake kuhusu kumpa kazi muhimu. Kwa mfano, je, Danieli aliwahi kusema uongo kwa mfalme au kumuibia? Walifikiri kwa muda mrefu na kwa bidii, lakini hawakuweza kupata chochote cha kumwambia Mfalme Dario. Walijua kwamba Danieli alikuwa mwaminifu na anaye aminika. ***(Danieli 6: 4)*** *Mtu anapoaminika ina maana kwamba wengine wanaweza kumtegemea kufanya kile anachosema atafanya. Elezea kuwa hii ndiyo njia ambayo Mungu anataka wafuasi wake wawe.*<br>• Maadui wa Danieli walipaswa kuja na njia ya kumfanya Danieli aonekane mbaya. Walijua kwamba mara nyingi alimuomba Mungu. Waliamua kumtegea Daniel mtego. Walimwendea Mfalme Dario na kumwomba atunge sheria mpya inayosema kwamba kwa siku 30 kila mtu lazima aombe kwa mfalme pekee. Ikiwa mtu atamwomba mtu mwingine, atupwe katika tundu la simba. Mfalme alikubali na kutia sahihi sheria mpya. ***(Danieli 6: 5-9)***<br>• Danieli alisikia kuhusu sheria mpya. Alijua ni mtego, lakini alimwamini Mungu atamlinda. Maombi yalikuwa muhimu sana kwake na ingawa alijua ni hatari, aliingia chumbani kwake na kusali mara tatu kwa siku kama alivyokuwa akifanya siku zote. Chukua muda kujadili maombi ni nini na umuhimu wake kwa Wakristo. Danieli alipokuwa akiomba, maadui zake walimuona. Wakaenda kumwambia mfalme kuhusu kile alichokuwa Danieli anakifanya. ***(Danieli 6: 10-13)***<br>• *Mfalme alikasirika sana! Hakutaka kumtupa Danieli katika tundu la simba bali sheria aliyokuwa ameitunga haingeweza kubadilishwa.* Hakuweza kufanya lolote kumsaidia Danieli. Mfalme akaamuru Danieli aletwe na kutupwa katika tundu la simba. Alimwambia Danieli kwamba Mungu ambaye alimtumikia daima angeweza kumwokoa. ***(Daniel 6: 14-16)*** *Jadili na watoto kile wanachofikiri kitatokea baadaye. Ni nani awezaye kumwokoa Danieli?*<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Danieli: Dirisha lililofunguliwa. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na kuelezea Mstari Muhimu ambao ni sehemu ya habari – ***Danieli 6: 16***. |
| **KUMBUKA** | Andika maneno yafuatayo kwenye ubao au kipande cha karatasi. Waambie watoto wachambue tabia njema kutoka kwenye zile mbaya.<br>Mwaminifu mwenye wivu mwenye bidii ya kazi anayeaminika anayetamani vya wengine anayesimulia hadithi mwenye chuki mwombaji mkweli<br><br>Wakumbushe watoto kwamba Mungu anaweza kufanya kazi ndani yetu ili maisha yetu yampendeze. |

<u>C1 Habari ya Nne</u>

**Danieli - Katika tundu la simba – Habari hii inahusu kumthibitisha Mungu kuwa ni mwaminifu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Danieli alimtumikia Mungu kwa uaminifu.<br>• Mungu ni Mungu anayeponya na kuokoa.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Danieli 6: 22***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Danieli 6: 17-28*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Waambie watoto wajadili habari iliyotangulia wakiwa wawili wawili. Je, wanaweza kutoa majibu kwa ajili ya maswali yafuatayo?<br>Je, Danieli alikuwa mzuri katika kazi yake? Mfalme Dario alitaka kumfanyia nini Danieli? Kwa nini maadui wa Danieli walimwonea wivu? Kwa nini Danieli alitupwa katika tundu la simba? Je, ni kweli Mfalme Dario alitaka Danieli atupwe katika tundu la simba?<br>Uliza baadhi ya watoto wakuambie majibu yao. *Kisha jadili na watoto kile wanachofikiri kitatokea baadaye. Wakumbushe watoto kwamba Danieli alikuwa akimtumaini Mungu, hata katika hali hii ya hatari sana. Je, wanaweza kukumbuka mifano kama hiyo kutoka katika Habari ya Kwanza na ya Pili?* |
| **FUNDISHA** | • Danieli alitupwa katika tundu la simba. Mfalme akamwambia, Mungu wako unayemtumikia daima, atakuokoa. Jiwe liliwekwa mdomoni mwa hilo tundu na kutiwa muhuri. Mfalme akarudi ikulu. Hakula chochote, na hakuweza kulala. Alikuwa akimfikiria mtumishi wake mwaminifu na wa kuaminika, Danieli. ***(Daniel 6: 16-18)***<br>• Kesho yake asubuhi na mapema, mfalme aliamka na kwenda kwenye tundu la simba. Alimwita Danieli na kumuuliza kama Mungu wake aliweza kumwokoa kutoka kwenye simba hao.’ Mfalme alifurahi sana kusikia sauti ya Danieli. Danieli alijibu kwamba Mungu wake amemtuma malaika kufunga vinywa vya simba, ili wasimdhuru. Mungu alijua kwamba Danieli hakuwa amefanya kosa lolote hivyo akamlinda. *Jadili jinsi ambavyo mfalme alikuwa anajisikia sasa.* Mfalme Dario aliamuru kwamba Danieli atolewe katika lile tundu. Na badala yake aliamuru kwamba watu waliomshtaki Danieli kwa uovu watupwe ndani ya tundu la simba. ***(Danieli 6: 19-24)***<br>• Mfalme Dario aliwaandikia watu wote wanaoishi katika Ufalme wake. Aliwaamuru kumwamini Mungu aliye hai na kuwaambia jinsi Mungu alivyomwokoa Danieli kutoka kwenye simba. Aliwaambia kwamba Mungu ni Mungu anayeponya na kuokoa. ***(Daniel 6: 25-28)***<br>• *Mungu anaweza kutuokoa kutoka kwenye adhabu tunayostahili kwa kutenda dhambi zetu. Bwana Yesu alikufa msalabani, akachukua adhabu ya dhambi zetu. Ikiwa tunaamini kwamba alikufa kwa ajili yetu, Mungu atatusamehe na kutupa uzima wa milele.*<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Danieli katika tundu la simba. |
| **JIFUNZE** | Tumia Mstari Muhimu ili kusisitiza habari, na kukariri sehemu ya kwanza – ***Danieli 6: 22*** |
| **KUMBUKA** | **Daraja la Pili** - Mwalimu au mtoto anaweza kuchukua wajibu wa nafasi ya Danieli. Watoto wanamuuliza "Danieli" kuhusu kilichotokea na jinsi alivyojisikia.<br>**Daraja la Kwanza** - Watoto wangeweza kujifunza wimbo kuhusu Danieli. Danieli alikuwa mtu wa maombi” (Unaweza kuupata mtandaoni na vitendo vyake.) |

## C2 Habari ya Kwanza
**Kipofu aona – Habari hii inahusu Yesu kurejesha kuona kwa mtu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Yesu ni Mungu na anaweza kufanya mambo ya ajabu.<br>• Yesu anatusikia tunapoita.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 18: 43***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Luka 18: 35-43*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Waambie watoto wafunge macho yao na wajifanye kama hawawezi kuona. Wanajisikiaje? Waambie watoto kuwa wakati wa Yesu hapakuwa na msaada kwa mtu yeyote ambaye alikuwa kipofu, kuwa ombaomba kulikuwa ndio njia yao pekee ya kuishi. Hakuna aliyejali watu vipofu. Walakini, katika habari ya leo, tutasikia juu ya kujali ambako Yesu alikuwa nako kwa kipofu. |
| **FUNDISHA** | • Yesu alikuwa akisafiri kwenda Yerusalemu pamoja na wanafunzi wake. (Daraja la Pili - Unaweza kueleza kwamba alikuwa anaenda huko kufanya kazi ambayo Baba yake alimpa kufanya ya kufa msalabani.)<br>• Katika safari yao walifika mji uitwao Yeriko.<br>• *Zungumza kuhusu jinsi umati unavyokusanyika kama mtu muhimu anakuja.*<br>• Umati ulikuwa umekusanyika kumwona Yesu alipokuwa akiingia Yeriko. *Kwa nini walitaka kumwona Yesu?*<br>• Kando ya barabara kulikuwa na kipofu mmoja akiombaomba katika sehemu yake aliyozoea. Lakini leo alijua kuna kitu kinatokea! *Waulize watoto wachunguze jinsi alivyogundua kilichokuwa kikiendelea - nyayo, kelele, msisimko, kuuliza mtu na kuambiwa kwamba Yesu wa Nazareti alikuwa akipita.* ***(Luka 18: 35-37)***<br>• *Elezea msisimko wa mtu huyo na jinsi ambavyo hangeweza kunyamaza aliposikia kwamba ni Yesu.* Hakuweza kumwona Yesu, lakini aliweza kumwita kwa sauti kuu! Elezea jinsi alivyopaza sauti, “Yesu, Mwana wa Daudi, unirehemu.” Hii ilionyesha kwamba alitambua kwamba Yesu alikuwa ni nani - aliyetumwa na Mungu - na pia kwamba alijua Yesu angeweza kumsaidia kwa njia ambayo hakuna mtu mwingine angeweza kumsaidia. ***(Luka 18: 38)***<br>• Baadhi ya watu walijaribu kumnyamazisha. *Waambie watoto wajaribu kutafuta sababu. Zungumza kuhusu Yesu kuwa na muda kwa ajili ya kila mtu na jinsi anavyovutiwa na kila mmoja wetu.* Mtu huyo alidhamiria sana na akamwita tena Yesu. Yesu alimsikia na akaomba mtu huyo aletwe kwake. ***(Luka 18: 39-40)***<br>• Kisha Yesu akazungumza na mtu huyo - ***soma mstari wa 41***. Mtu huyo aliposema kwamba anataka kuona, alionyesha kwamba aliamini kwamba Yesu angeweza kufanya hivyo kwa ajili Yake. Yesu alifurahi kwamba mtu huyo alimwamini na kuonyesha imani Kwake. *Simulia jinsi Yesu alivyoweza kumponya upofu wake kwa kusema “Upate kuona.” Maneno ya Yesu yalikuwa na nguvu. Hakuna mtu mwingine angeweza kufanya hivi.* ***(Luka 18: 41-42)***<br>• *Waulize watoto kile ambacho mtu huyo aliona na hisia zake zilivyokuwa wakati Yesu alipompa kuona kwake. Umati uliitikiaje? Thibitisha majibu ya watoto kwa kusoma kile ambacho Biblia inasema.* ***(Luka 18: 43)***<br>• *Yesu anataka kuwasaidia watu na kuwatendea mema. Tunapofuata njia zetu wenyewe katika maisha yetu, ni kama kutembea gizani. Wakumbushe watoto kwamba Yesu ndiye Nuru ya Ulimwengu na tunapomfuata, tunatembea katika njia sahihi katika nuru.* ***(Yohana 8: 12)***<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Kipofu aona. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na kuelezea Mstari Muhimu – ***Luka 18: 43***. |
| **KUMBUKA** | Tumia maswali haya kwa ajili ya jaribio:<br>• Yesu alikuwa anakaribia mji gani?<br>• Nani alikuwa pamoja na Yesu?<br>• Nani alikuwa ameketi nje ya mji?<br>• Kwa nini mtu huyo alikuwa akiomba?<br>• Mtu huyo alimwitaje Yesu?<br>• Huyu mtu alitaka Yesu afanye nini?<br>• Mtu huyo alifanya nini Yesu alipomponya?<br>• Umati ulifanya nini? |

## C2 Habari ya Pili

**Umati walishwa – Habari hii inahusu Yesu kuwalisha watu wenye njaa.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Yesu pekee ndiye aliweza kukidhi hitaji la umati huu wenye njaa.<br>• Yesu ndiye Mkate wa Uzima na anaweza kutupa uzima wa milele.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 6: 35***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Yohana 6: 1-14*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Daraja la Kwanza - Panga safari ya kuigiza ya matembezi na watoto. Nani angetakiwa kuwepo, mngekula nini na mngeenda wapi kula?<br>Daraja la Pili - Zungumza kuhusu kwenda kusikiliza au kutazama mtu maalumu akiongea, akiimba, akiigiza n.k. Mtu huyo anaweza kuwa maarufu, lakini baada ya muda fulani ungejisikiaje? Labda uchovu, kupoteza shauku, kujisikia joto au wasiwasi. Yesu alikuwa anaenda kuwaonyesha umati na wanafunzi wake kwamba anaweza kuwapa mahitaji yao yote. |
| **FUNDISHA** | • Yesu alitaka kupata muda wa kuwa pamoja na wanafunzi wake na kuwafundisha mambo muhimu kuhusu Mungu. *Elezea mpangilio – mahali pa utulivu milimani.* Lakini hata huko, watu wengine walienda na kuwakuta. *Waulize watoto watafakari kwa nini watu walienda kumtafuta Yesu.* Muda mfupi baadaye, umati mkubwa sana ulikuwa umekusanyika. ***(Yohana 6: 1-3)***<br>• *Yesu alijisikieje watu wengine walipoungana nao?* Elezea kuwa Yesu hakutaka kuwafukuza watu hawa. Walikuwa muhimu Kwake pia na Yeye aliwahurumia. ***(Mathayo 14: 14)***<br>• Akamwuliza swali Filipo, mmoja wa wanafunzi wake, Tununue wapi mikate ili watu hawa wale? Elezea kwamba Yesu alitaka kumjaribu Filipo ili kuona kama aliamini kwamba Yesu angeweza kusaidia. *Je! watoto wangejibuje?* Philipo hakuweza kuona njia ya kutatua tatizo; alisema kwamba ingechukua mshahara wa mtu wa nusu mwaka na kila mtu katika umati angepata kipande kimoja tu cha mkate. ***(Yohana 6: 5-7)***<br>• Andrea aligundua mvulana katika umati ambaye alikuwa na chakula cha mchana na kumleta kwa Yesu.<br>• *Kwa watoto wa Daraja la Kwanza, pata sanduku la chakula cha mchana na ulifungue ili kufunua mikate mitano midogo na samaki wawili waliokatwa.* Kama alivyosema Filipo, Andrea pia alijua kwamba chakula hicho hakitoshi.<br>• *Waulize watoto kama wanaweza kufikiria mtu ambaye angeweza kutoa chakula kwa umati mkubwa. Endelea kuelezea jinsi Yesu alivyotimiza mahitaji ya kila mtu, ukizungumzia dondoo zifuatazo:* ***(Yohana 6: 8-9)***<br>• Aliwaambia wanafunzi wawaketishe watu.<br>• Alimshukuru Mungu kwa chakula hicho. *(Maombi - ni muhimu kwetu kukumbuka kwamba chakula chetu kinatoka kwa Mungu.)*<br>• Aligawa chakula, wakapewa, na kila mtu akashiba.<br>• Hakuna kilichoharibika – vikapu 12 vilibaki. *(Matumizi ya ujumbe huu - hatupaswi kuharibu chakula.)*<br>• *Onyesha mshangao kuwa kulikuwa na chakula cha kutosha kwa ajili ya kila mtu – umati wa watu zaidi ya 5000! Jaribu kuweka idadi hii katika muktadha wa watoto.* Watu walikuwa wanaanza kufikiri kwamba Yesu ndiye Masihi aliyeahidiwa aliyetumwa kutoka kwa Mungu kwa kuwa hawakuwa wamewahi kuona jambo kama hilo hapo awali. ***(Yohana 6: 10-14)***<br>• Baadaye, Yesu alizungumza na wanafunzi wake kuhusu kile kilichotokea. Aliwaambia kuhusu kuitwa “Mkate wa Uzima.” Yesu alikuwa amekidhi njaa ya watu, lakini Anaweza kufanya mengi zaidi. Yeye ndiye mpaji wa uzima wa milele... hiyo ina maana kwamba Anaweza kutupa maisha bora zaidi ambayo hutuleta katika familia ya Mungu. ***(Yohana 6: 35)***<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Umati walishwa. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na kuelezea Mstari Muhimu – ***Yohana 6: 35*** |
| **KUMBUKA** | Tumia maswali haya kwa ajili ya jaribio:<br>• Yesu na wanafunzi wake walikuwa wapi?<br>• Kwa nini watu wengi walitaka kumwona Yesu?<br>• Filipo alisema nini Yesu alipomtaka anunue mkate?<br>• Mvulana mdogo alikuwa na chakula gani?<br>• Yesu alilisha watu wangapi?<br>• Vikapu vingapi vilibaki?<br>• Yesu aliwaambia wanafunzi wake kuwa yeye ni nani?<br>• Kichwa hiki kinatufundisha nini kuhusu kile ambacho Yesu anaweza kutoa? |

## <u>C2 Habari ya Tatu</u>

## Kiwete atembea – Habari hii inahusu watu kuelewa Yesu ni nani hasa.

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Yesu alikuwa na uwezo wa kumfanya mtu atembee...<br>• Yesu pekee ndiye anayeweza kusamehe dhambi zetu.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 5: 24***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Yohana 5: 1-15*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Waombe watoto washirikishe uzoefu wa kuvunjika mguu au kupata jeraha kama hilo. Zungumza kuhusu jinsi inavyokuwa mtu anapowategemea wengine badala ya kujituma kufanya kazi yeye mwenyewe. Walikuwa na vifaa gani vya kuwasaidia? k.m., magongo, kiti cha magurudumu cha walemavu.<br>Tafakari juu ya huyu mtu katika habari ya leo - miaka 38 ya kutoweza kutembea na kuishi katika wakati ambapo hapakuwa na mpango wowote wa kusaidia ulemavu wake na hapakuwa na marafiki wa kusaidia! Darasa linaweza kujua kuhusu shirika la hisani linalosaidia watu wenye ulemavu na kuhusika kwa vitendo. Muda wote uwe mwangalifu kwa hali maalum ambazo watoto wanapaswa kushughulika nazo katika familia zao. |
| **FUNDISHA** | • **Yesu kwenye Birika -** Yesu alikuwa anatembelea Yerusalemu kwa ajili ya karamu maalumu. ***(Yohana 5: 1)***<br>• Kulikuwa na birika huko Yerusalemu, na watu waliamini wakati maji yake yanapochemka mtu wa kwanza kuingia ndani ya maji angeponywa. Vipofu wengi, viwete na waliopooza walikuwa wamelala karibu na birika.<br>• *Jadili jinsi ambavyo watu hawa walijisikia. k.m., wenye matumaini, msisimko, wenye wasiwasi, waliokatishwa tamaa, wasio na tumaini...* Yesu alifika kwenye birika na kupata habari kwamba mtu aliyekuwa kilema alikuwa amekaa humo kwa miaka 38. *(Hakikisha kwamba watoto wanaelewa kuwa kiwete hakuweza kutembea).* Yesu aliendа kuongea naye na kumuuliza kama alitaka kupona.<br>• Mlemavu huyo alieleza kuwa hangeweza kuingia ndani ya maji kwani hakuwa na mtu ambaye angeweza kumsaidia. *Soma mazungumzo katika* ***mstari wa 7 na 8****.* Mtu huyo alikuwa hana matumaini kabisa. ***(Yohana 5: 5-8)***<br>• *Kazia kwamba Yesu alikuwa akimwagiza mtu huyo afanye jambo ambalo hakuweza kufanya kwa miaka 38!* Yesu alipomwambia asimame huyo mtu akapewa uwezo wa kutembea. Yule mtu akapona mara, akasimama, akachukua godoro lake, akaenda zake. ***(Yohana 5: 8-9)***<br>• **Wayahudi waona kosa -** *Eleza kwamba mtu huyo aliponywa siku ya Sabato. (Jumamosi yetu) Wayahudi walikuwa na sheria nyingi kuhusu kile ambacho hawakuweza kufanya siku hii.* Waliona ni kosa kwa mtu huyo kubeba godoro lake. Alisema kwamba mtu aliyemponya alimwambia afanye hivyo, lakini pia alikiri kwamba hakujua mtu huyo alikuwa nani. ***(Yohana 5: 10-12)***<br>• **Yesu Hekaluni** - ***(Yohana 5: 14-15)*** Baadaye, Yesu alimwona mtu huyo tena Hekaluni na akazungumza naye, akimwambia usitende dhambi tena. *Eleza "kutenda dhambi" ni nini –* kwamba sisi sote tunamkosea Mungu kwa mambo tunayofikiri, tunayosema, na kufanya. Mtu huyo alikuwa na mahitaji mawili tofauti, kuweza kutembea na kusamehewa dhambi yake. Hakuwa ameelewa ipasavyo kuhusu Yesu pale mwili wake ulipoponywa, lakini sasa alikuwa akipewa fursa ya kujifunza zaidi kwamba Yesu ni nani na kile ambacho angeweza kumfanyia.<br>• *Elezea kwamba Bwana Yesu ndiye pekee anayeweza kusamehe dhambi zetu. Tunahitaji kusamehewa dhambi zetu, ili maisha yetu yampendeze Mungu na tuweze kuishi kwa ajili ya kumtumikia.*<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Kiwete atembea. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na kuelezea Mstari Muhimu – ***Yohana 5: 24*** |
| **KUMBUKA** | Tumia maswali haya kwa ajili ya jaribio:<br>• Yesu alikuwa katika mji gani?<br>• Kwa nini watu hawa wote wagonjwa na waliojeruhiwa walikuwa wamelala karibu na birika?<br>• Kwa nini mtu huyo alikuwa huko kwa muda mrefu?<br>• Yesu alimwambia mtu huyo afanye nini?<br>• Kwa nini Wayahudi hawakufurahishwa na mtu huyo?<br>• Yesu alimwona wapi tena mtu huyo?<br>• Alimwambia mtu huyo afanye nini wakati huu?<br>• Mtu huyo hakuelewa nini kuhusu Yesu? |

## C2 Habari ya Nne

**Msichana aliyekufa afufuka! – Habari hii inahusu Yesu kutoa maisha mapya.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Yesu huwasaidia wale wanaokuja kwake.<br>• Hakuna jambo gumu kwa Yesu kulifanya.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Marko 5: 42***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Marko 5: 21-43*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Zungumza kuhusu watu muhimu katika jamii unayoishi - k.m., watoto wanaweza kutambua cheo/kazi ya mtu anayesimamia serikali, mahakama, polisi, ukumbi wa jiji n.k. Habari ya leo ni kuhusu mtu muhimu ambaye alihitaji kuomba msaada. Kuomba msaada si rahisi kila wakati hasa kama wewe ni mtu maarufu. |
| **FUNDISHA** | • Bwana Yesu alizungukwa tena na umati wa watu. Huu ulikuwa ni umati mkubwa wa watu waliosongana na kusukumana na kufanya iwe vigumu sana kusogea.<br>• Lakini wakati huo huo umati wa watu ukasogea pembeni mtu fulani mkuu kutoka mjini alipokuja kumwona Yesu. Elezea kwamba Yairo alikuwa mtawala katika sinagogi kumaanisha kwamba kila mtu katika eneo hilo angemjua yeye ni nani. ***(Marko 5: 22-23)***<br>• Ghafla mtu huyu muhimu, ambaye alizoea kutoa maagizo, alianguka miguuni pa Yesu na kuomba msaada Wake.<br>• *Elezea kuwa hii haikuwa hali ya kawaida kwani wengi wa wakuu wa sinagogi hawakumpenda Yesu au mafundisho Yake na wangeweza tu kupiga magoti mbele za Mungu na bila shaka si mbele ya mtu aliye hai.*<br>• Yairo alikata tamaa. Binti yake alikuwa mgonjwa sana, na aliamini kabisa kwamba Yesu angeweza kumponya. Matendo yake na maneno yake yanatuonyesha aliamini Yesu alikuwa ametoka kwa Mungu. Yesu alikuwa tayari kumsaidia Yairo. Elezea kuwa Yeye huwasaidia wote wanaokuja Kwake. ***(Marko 5: 23)***<br>• Wakiwa njiani ujumbe ulikuja kuwa mtoto amefariki. Yesu alizungumza na Yairo na kumwambia awe na imani. Walienda hadi kwenye nyumba ambayo kulikuwa na kelele na kilio. Yesu aliwatoa nje ya nyumba na kuchukua wanafunzi wake watatu na wazazi wake hadi ndani ya chumba. ***(Marko 5: 38-40)***<br>• Yesu alisema na msichana huyo na kumwambia ainuke. Aliinuka na kuanza kutembea huku na kule. Elezea kuwa alikuwa amekufa na kisha Yesu akamfufua. Hakuwa mzimu wala kitu kingine. Msichana akawa mzima kabisa; akaweza kutembea na kuzungumza na kula. ***(Marko 5: 41-43)***<br>• *Elezea kuwa tunapaswa kushukuru kwa ajili ya zawadi ya uzima na kufikiria kwamba ni jambo la ajabu kuwa hai na kufurahia mambo mazuri ambayo Mungu ametupa. Bwana Yesu pia anataka kutupa aina nyingine ya uzima - uzima wa milele tunapomtumainі. Hapo ndipo tutajua kwamba dhambi zetu zimesamehewa, maisha yetu yanakubalika kwa Mungu na siku moja tutakuwa Mbinguni - Angalia* ***Warumi 6: 23****.*<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Msichana aliyekufa afufuka. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na kuelezea Mstari Muhimu – ***Marko 5: 42***. |
| **KUMBUKA** | Tumia maswali haya kwa ajili ya jaribio:<br>• Nani alikuja kumwona Yesu?<br>• Kwa nini Yairo alikuwa mtu maarufu?<br>• Alifanya nini ambacho hakikuwa cha kawaida?<br>• Nini kilitokea walipokuwa njiani?<br>• Waliona nini nyumbani?<br>• Yesu aliingia nyumbani na akina nani?<br>• Yesu alipozungumza na msichana alifanya nini?<br>• Je, Yesu anaweza kutupa maisha ya aina gani? |

## C3 Habari ya Kwanza

**Zakayo – Habari hii inahusu Zakayo kumpokea Yesu kama Mwokozi wake.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Maisha ya Zakayo yalibadilika alipokutana na Yesu.<br>• Bwana Yesu anataka kuwa Mwokozi na Rafiki yetu.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 19: 9***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Luka 19: 1-10*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Zungumza kuhusu jinsi mji wako ulivyokaribisha mgeni au shujaa muhimu. Labda watoto wanaweza kusimulia uzoefu wao. Zingatia mazingira, kelele na kile kilichoweza kuonekana. |
| **FUNDISHA** | • Watu wa Yeriko walikuwa wamesikia habari za Yesu. *Walisikia kuhusu nini? Alikuwa mwalimu na mponyaji mzuri… Fikiria tena habari katika C2.*<br>• Yesu alipokuwa akipita katikati ya mji akielekea Yerusalemu, umati mkubwa wa watu ulimsonga Yesu ili kuona kile ambacho angefanya na kusema baadaye. Mtu mmoja aliyetaka kumwona Yesu alikuwa anaitwa Zakayo, mtu tajiri, na mkuu wa watoza ushuru katika mji huo. *Waulize watoto kwa nini watu hawakumpenda mtoza ushuru. Elezea kuwa Zakayo hakuwa mwaminifu kwa sababu alichukua pesa nyingi sana kutoka kwa watu na akajiwekea baadhi kwa ajili yake binafsi.* ***(Luka 19: 1-2)***<br>• Zakayo alipojaribu kumwona Yesu, alikuwa na tatizo. Alikuwa mfupi sana na hangeweza kuona juu ya vichwa vya umati wa watu. *Onyesha kitendo cha kunyanyuka ili uone juu ya vichwa vya watu.* ***(Luka 19: 3)***<br>• Zakayo alipata wazo! Alikimbia mbele ya Yesu na kupanda kwenye mti wa mkuyu ili aweze kumwona. Lakini, Yesu alipopita chini ya mti, alitazama juu. akamwona Zakayo. *Onyesha mshangao wa Zakayo kwamba Yesu alisimama kando yake... Waambie watoto kile Yesu alichosema.* Zakayo alifurahi sana! Alishuka kutoka kwenye mti na kumpeleka Yesu nyumbani kwake. ***(Luka 19: 4-6)***<br>• Umati ulinung'unika kwa sababu Yesu alikuwa ameenda kwenye nyumba ya mwenye dhambi. *Elezea kuwa walifikiri Yesu angejiweka mbali na wenye dhambi.* Walikuwa wakimwita Zakayo kuwa ni mwenye dhambi. *Jadili neno "mwenye dhambi" na ukweli kwamba sisi sote ni wenye dhambi.* Dhambi hututenganisha na Mungu. Zakayo alisikiliza yale ambayo Yesu alisema na alijua kwamba alipaswa kubadilika. Alitaka kuishi kwa ajili ya Mungu na si kwa ajili yake mwenyewe. Ili kuonyesha kwamba alijuta sana kwa kuchukua pesa ambazo si zake, alimwambia Yesu kwamba angetoa nusu ya fedha zake kwa maskini na kulipa pesa nyingi zaidi kuliko alizochukua kimakosa. ***(Luka 19: 7-8)*** Mtu yeyote ambaye ni rafiki na mfuasi wa Yesu atataka kumtii Mungu na si kuwaibia wengine. ***(Kutoka 20: 15)***<br>• Yesu alimwambia Zakayo kwamba "Wokovu umefika nyumbani humu." Mabadiliko ya kweli yalifanyika katika maisha yake kwa sababu Yesu alikuwa amemwokoa kutoka kwenye dhambi yake. Kuanzia sasa na kuendelea, namna ambavyo angefanya kazi yake na kuwatendea wengine ingekuwa tofauti kabisa. ***(Luka 19: 9-10)***<br>• *Yesu alikuja kutuokoa kutoka kwenye dhambi zetu pia. Ikiwa tunaomba msamaha kwa Mungu kwa makosa ambayo tumefanya, ameahidi kutusamehe dhambi zetu na tunakuwa sehemu ya familia ya Mungu. Tutataka kuishi maisha yanayopendeza Mungu.*<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Zakayo |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na kuelezea Mstari Muhimu – ***Luka 19: 9.*** Zakayo alikuwa mwana wa Ibrahimu si kwa sababu tu alikuwa Myahudi, lakini kwa sababu, kama Ibrahimu, sasa alimpenda Mungu na angeishi maisha yake ili kumpendeza. Alifanyaje hivyo katika habari ya leo? |
| **KUMBUKA** | Tumia maswali haya kwa ajili ya jaribio:<br>• Yesu alikuwa anaenda wapi?<br>• Alikuwa akipitia mji gani?<br>• Kazi ya Zakayo ilikuwa nini?<br>• Kwa nini watu walimchukia?<br>• Zakayo alipaswa kufanya nini ili amwone Yesu?<br>• Ni nani walinung'unika Yesu alipoenda nyumbani kwa Zakayo?<br>• Zakayo alionyeshaje kwamba maisha yake yalikuwa yamebadilika kwa kukutana na Yesu?<br>• Aliahidi kufanya nini?<br>• Yesu alitoa sababu gani ya kuja kwake?<br>Au darasa linaweza kuigiza hadithi. Mwalimu angeweza kusoma kifungu cha Biblia na watoto kuchukua sehemu za Yesu, Zakayo, na umati. |

## C3 Habari ya Pili

**Nikodemo – Habari hii inahusu kuwa na uzima wa milele.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Nikodemo alitaka kujifunza zaidi kuhusu Yesu.<br>• Tunahitaji kuzaliwa mara ya pili ili tuwe na uzima wa milele.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 3: 16***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Yohana 3: 1-16*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Daraja la Kwanza - Kuwa na picha ya mtoto na kuzungumza juu ya ajabu ya maisha mapya.<br>• Daraja la Pili - Farisayo ni nani? *Elezea kuwa walikuwa ni kikundi cha viongozi wa kidini katika wakati wa Yesu ambao walifikiri kwamba kwa kushika sheria na mapokeo ya Kiyahudi wangekuwa na uzima wa milele.* Katika habari ya leo Farisayo alikuwa na hamu ya kujitafutia ukweli. |
| **FUNDISHA** | • Yesu alikuwa Yerusalemu kwa ajili ya sikukuu ya Pasaka. Mwanaume muhimu katika jiji hilo, Nikodemo, alitaka kujua mengi zaidi kuhusu Yesu. *Elezea kuwa ni jambo zuri kutaka kujua zaidi kuhusu Yesu.* Alikuwa amesikia Yesu amefanya miujiza na kufundisha watu juu ya Mungu. Nikodemo alikuwa Farisayo. (Daraja la Pili) Aliamua kwenda kumwona Yesu usiku. *Zungumza kwa nini aliendа usiku - labda hakutaka kuonekana au alitaka kwenda kukiwa na watu wachache karibu na Yesu. Soma aliyomwambia Yesu.* ***(Yohana 3: 1-2)***<br>• Yesu alimwambia Nikodemo kwamba watu wanahitaji 'kuzaliwa mara ya pili' ili wapate uzima wa milele. Nikodemo alishangaa. *Soma **Yohana 3: 4** na uwasaidie watoto kuelewa tatizo la Nikodemo.* Yesu alieleza kwamba haitoshi kuzaliwa kama mtoto, bali tunahitaji aina mpya ya maisha. Tuna maisha haya mapya tunapomwomba Mungu atusamehe dhambi zetu na kufuata yale ambayo Mungu anasema katika Biblia. *Elezea kuwa tunapozaliwa, sisi ni sehemu ya familia, lakini tunapokuwa na maisha mapya ya Mungu ni kama kuzaliwa tena katika familia mpya, familia ya Mungu, na tunakuwa watoto wa Mungu.* ***(Yohana 3: 3-4)***<br>• *Ukiwa na watoto wa Daraja la Pili unaweza kuzungumza juu ya jukumu la Roho Mtakatifu. Yesu alimlinganisha na upepo. Hatuwezi kuona upepo, lakini tunaweza kuona kile unachofanya. Waulize watoto kwa mifano. Roho Mtakatifu haonekani pia, lakini Anafanya kazi wakati mtu anapoelewa kuhusu kuhitaji kuzaliwa katika familia ya Mungu. Roho Mtakatifu ndiye Msaidizi na Kiongozi ambaye yuko hai na anayefanya kazi katika maisha ya Mkristo* ***(Yohana 3: 5-8)***<br>• Yesu alishangaa kuwa Nikodemo hakuelewa alichokuwa akisema. Ilikuwa vigumu kwa Nikodemo kuelewa mambo kuhusu Mbingu lakini Yesu alieleza kwamba Mwana wa Adamu (Yeye Mwenyewe) alikuwa amekuja kutoka Mbinguni. ***(Yohana 3: 9-13)***<br>• *Kisha Yesu akaendelea kumkumbusha Nikodemo wakati ambapo Mungu alimwambia Musa kuweka nyoka wa shaba juu ya mti jangwani ili Waisraeli waweze kuokolewa na kifo. (B 11 Habari ya Nne:* ***Hesabu 21: 4-9****) Ukiwa na Daraja la Pili unaweza kuingia kwa undani zaidi. Yesu alieleza kwamba Yeye pia angeinuliwa .... msalabani ili kila mtu amwaminiye apate kuokolewa na dhambi.* ***(Yohana 3: 14-15)***<br>• *Kinachofuata labda mstari unaojulikana sana katika mistari ya Biblia na Mstari Muhimu.* ***(Yohana 3: 16)*** *Zungumza na watoto kuhusu habari njema ya Mungu.* Yesu alimwambia Nikodemo kwamba Mungu anampenda kila mtu ulimwenguni kiasi kwamba alimtuma Mwanawe, Yesu, afe msalabani.<br>• *Kila mtu anayemwamini Yesu na kifo chake kama njia ya kuchukua adhabu ya dhambi, anaweza kuwa na uzima wa milele na siku moja kuwa Mbinguni.*<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Nikodemo. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na kuelezea Mstari Muhimu – ***Yohana 3: 16***, Onesha watoto muundo wa mstari, ukionesha sehemu katika rangi tofauti. Nusu ya kwanza inatuambia juu ya Mungu - Yesu, Mwana yuko katikati - nusu ya pili inatuambia kile tunachohitaji kufanya. |
| **KUMBUKA** | Badili maswali ya jaribio kwa maudhui uliyoshughulikia. Au watoto wanaweza kueleza baadhi ya mambo ambayo Yesu alimfundisha Nikodemo. k.m.<br>• Mtoto mpya na wazazi/ kuzaliwa katika familia ya Mungu.<br>• Upepo/Roho Mtakatifu.<br>• Nyoka juu ya mti/ Yesu msalabani.<br>• Upendo wa Mungu kwa ulimwengu. Kusanya picha za watoto wa mataifa tofauti na uziweke kwenye ramani. Yohana 3:16 imeongezwa kama nukuu. |

## C3 Habari ya Tatu

**Mwanamke kutoka Samaria – Habari hii inahusu Yesu kutoa 'maji yaliyo hai'.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Yesu alitumia muda kumweleza mwanamke kuhusu kile alichohitaji zaidi kuliko vyote.<br>• Yesu anaalika kila mtu kupokea "maji yaliyo hai".<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 4: 42***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Yohana 4: 4-30, 39-42*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Ni nini kinakufanya uwe na kiu? Waulize watoto watoe maoni yao. Ni jambo gani bora zaidi la kukata kiu yako? Zungumza kuhusu mahali unapoenda kupata maji. (bomba, maji baridi yaliyohifadhiwa kwenye friji, chupa ya maji ya shule, chemchemi ya maji ya kunywa, kisima) Zungumza kuhusu jinsi maji yanavyotuliza kiu kwa muda ... lakini baada ya muda utapata kiu tena. Katika habari ya leo Yesu anaomba maji ya kunywa! Alikuwa binadamu na alisikia kiu kama sisi.<br>• Au unafanya nini unapopata habari njema? *Waulize watoto kwa mifano na kama wanapenda kuwaambia wengine.* Mwanamke katika habari yetu alikuwa na habari njema za kuwaambia majirani na marafiki zake. |
| **FUNDISHA** | • Yesu alikuwa safarini pamoja na wanafunzi wake akaamua kupitia Samaria. *Onyesha kwenye ramani ya Biblia kwa watoto wakubwa zaidi.* Alifika katika mji uitwao Sikari. Yesu, aliyekuwa anajisikia joto na kuchoka, aliketi karibu na kisima. *Kwa Daraja la Kwanza, toa maelezo zaidi au kielelezo cha kisima.* Ilikuwa saa sita ya mchana. Wafuasi wake walikuwa wameenda kununua chakula mjini, kwa hiyo Yesu alikuwa peke yake. ***(Yohana 4: 4-6)***<br>• Alipokuwa ameketi pale, mwanamke mmoja alifika kisimani na mtungi kuteka maji. *Elezea kwa nini jambo hili halikuwa la kawaida – ilikuwa kawaida kuteka maji wakati wa jioni.* Yesu alimwomba maji ya kunywa. *Elezea kwa nini mwanamke huyo (Msamaria) alishtuka kwamba Yesu (Myahudi) alikuwa anazungumza naye. Wayahudi na Wasamaria hawakuwa na mahusiano mazuri.* ***(Yohana 4: 7-9)***<br>• Yesu alimwambia mwanamke huyo kwamba angeweza kumpa 'maji yaliyo hai' na hangeona kiu tena. Mwanamke hakuelewa kwa sababu Yesu hakuwa na mtungi wowote wa kutekea maji kutoka kisimani. *Elezea kuwa Yesu hakuwa akizungumza kuhusu maji ya kisimani bali jinsi ambavyo angeweza kutoa uzima wa milele au 'maji yaliyo hai'.* ***(Yohana 4: 10-15)***<br>• Yesu alimwambia mwanamke huyo kwamba alijua yote kuhusu mambo mabaya ambayo alikuwa amefanya zamani. *(Sema maneno yanayoendana na umri wa watoto unaowafundisha.)* Mwanamke alishangaa kwamba Yesu alijua mengi kuhusu maisha yake! Alitambua kuwa hakika alikuwa nabii aliyetoka kwa Mungu. Baada ya mazungumzo mengine zaidi, Yesu alimwambia mwanamke huyo kwamba Yeye ndiye ambaye Mungu aliahidi kumtuma ili kuwaokoa watu kutoka katika dhambi zao. ***(Yohana 4: 16-26)*** *Eleza kwamba wale wanaoamini kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu na kumwomba awasamehe dhambi zao siku moja wataenda Mbinguni - watapata uzima wa milele.*<br>• Wakati huo huo, wafuasi wa Yesu wakarudi. Mwanamke huyo alifurahishwa sana na yale ambayo Yesu alisema kiasi kwamba aliacha mtungi wake karibu na kisima na kukimbia ili kuwahubiria wengine habari njema. *Soma alichosema.* ***(Yohana 4: 29)***. Watu kutoka mjini wakatoka kwenda kumwona Yesu. ***(Yohana 4:27-30)***<br>• Walipokuwa wakimsikiliza Yesu, Wasamaria wengi walimwamini. Walitambua Yeye ni nani. ***(Yohana 4: 39-42)*** *Soma Mstari Muhimu ambao unatuambia kile walichoamini hasa. Je, unamjua Bwana Yesu kama Mwokozi wako? Je, umeomba msamaha kwa kufanya mabaya na ukaamua kufanya yale ambayo Mungu anasema katika Biblia? Ikiwa umefanya hivyo, kwa nini usishirikishe habari njema kwa wengine, kama yule mwanamke kisimani alivyofanya?*<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Mwanamke kutoka Samaria. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na kuelezea Mstari Muhimu – ***Yohana 4: 42***, au sehemu ya mwisho kwa watoto wadogo. *Eleza kwamba 'ulimwengu' maana yake ni watu wanaoishi ndani yake.* |
| **KUMBUKA** | Tumia maswali haya kwa ajili ya jaribio:<br>• Yesu alisimama wapi katika safari yake?<br>• Alikutana na nani?<br>• Aliomba nini?<br>• Badala yake alimpa mwanamke nini?<br>• Yesu anawapa nini wale wanaompenda?<br>• Kwa nini mwanamke huyo alikimbia na kuacha mtungi wake?<br>• Nani walikuja kumwona Yesu?<br>• Je, waliamini kwamba Yesu ni nani? |

## C3 Habari ya Nne

**Kijana tajiri – Habari hii inahusu kumpa Bwana Yesu nafasi ya kwanza.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Yesu alijibu swali kuhusu jinsi ya kupata uzima wa milele.<br>• Yesu anataka kupewa nafasi ya kwanza katika maisha yetu.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Marko 10: 21***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Marko 10: 17-23*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Waulize watoto wazungumzie jambo ambalo ni muhimu zaidi kwao - labda mdoli maalum, kifaa fulani, kitu anachopenda au mbwa. Pengine wamewahi kufanya "Onyesha na Kusema" kuhusiana na mada hii. Elezea kuwa wana bahati sana kuwa na vitu hivi ambavyo wanafurahia sana kuwa navyo. Ni vitu vyema ambavyo Mungu amewapa. Lakini baada ya muda kupita, pengine vinaweza kubadilishwa. Ni muhimu kwamba Yesu Mwenyewe ana maana zaidi kwetu kuliko vitu vingine vyote tulivyo navyo. Anatupenda na anatujali sana na ndiye rafiki bora zaidi tunayeweza kuwa naye.<br>• Wakumbushe/ongea na watoto kuhusu sheria za Mungu. Je! ni amri gani ya kwanza kati ya amri kumi ***(Kutoka 20: 3)*** - "Usiwe na miungu mingine ila mimi". Hii ina maana gani? Mungu anapaswa kuwa na nafasi ya kwanza katika maisha yetu. |
| **FUNDISHA** | • Siku moja, kijana mmoja tajiri alikuwa na swali muhimu la kumuuliza Yesu. Kwa hiyo, alikimbia kumfuata Yesu alipokuwa akitembea barabarani akampigia magoti. *Unafikiri ni kwa nini alipiga magoti mbele za Yesu? (Alijua Yesu alikuwa mtu muhimu) Elezea kile alichouliza.* Sasa kijana huyu alikuwa na pesa nyingi na angeweza kununua nguo zote zilizo bora, kuishi katika nyumba kubwa, na kuwa na vitu vyote alivyotaka. Lakini, pamoja na hayo yote, alitaka kujua anaweza kufanya nini ili kuwa na uhakika kwamba siku moja angeenda Mbinguni. ***(Marko 10: 17)***<br>• Yesu hakujibu swali lake kwa njia ya moja kwa moja. Yesu alimkumbusha kijana huyo baadhi ya sheria za Mungu. *Je, unaweza kukumbuka zinaitwaje? (Amri 10) Waulize watoto kama wanaweza kukumbuka amri yoyote ambayo inaeleza jinsi tunavyopaswa kuwatendea watu wengine. Taja zile ambazo Yesu aliziorodhesha.*<br>• Kijana huyo alimwambia Yesu kwamba alikuwa ameshika amri hizi zote tangu alipokuwa kijana. ***(Marko 10: 18-20)*** *Eleza kwamba kijana huyo hakudhanii kwamba alikuwa amefanya kosa. Hakujua kwamba alikuwa mtenda-dhambi na alikuwa amevunja sheria za Mungu. Sisi sote tumevunja amri za Mungu. Hakuna mtu ambaye ni mkamilifu, isipokuwa Yesu peke Yake.*<br>• Yesu alimtazama kijana huyo na kumpenda. Kisha alimpima kijana huyo ili kuona kama alikuwa na nia ya kutaka uzima wa milele. Hii ilimaanisha kwamba siku moja angeenda Mbinguni na kuishi milele na Mungu. *Elezea kile ambacho Yesu alimwambia afanye. Elezea kuwa 'hazina Mbinguni' ilimaanisha kwamba siku moja kijana huyo angekuwa na uzima wa milele.* Yesu alitaka kuona ikiwa pesa za kijana huyu na vitu vyote alivyokuwa navyo vilikuwa muhimu zaidi kwake kuliko kumfuata Yeye. ***(Marko 10: 21)***<br>• Biblia inatuambia kwamba uso wa kijana huyo ulionekana kuwa na huzuni. Mtihani ulikuwa mgumu sana. Hakutaka kutoa vyote alivyokuwa navyo kwa sababu alikuwa tajiri sana. Aliondoka zake na hakuwa mfuasi wa Yesu. Hakuona kwamba kumpa Yesu nafasi ya kwanza ni jambo la maana zaidi maishani mwake. Kijana huyo alipokuwa ameondoka, Yesu aliwaambia wafuasi wake kwamba ni vigumu sana kwa mtu tajiri kuwa mmoja wa wafuasi Wake na kuwa sehemu ya ufalme wa Mungu kwa sababu wanapenda zaidi walicho nacho duniani kuliko Yesu.<br>• *Je, umempa Yesu nafasi ya kwanza katika maisha yako?* ***(Marko 10: 22-23)***<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kijana tajiri. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na kuelezea Mstari Muhimu – ***Marko 10: 21***, au sehemu yake kwa watoto wadogo. |
| **KUMBUKA** | Tumia maswali haya kwa ajili ya jaribio:<br>• Kijana huyo alionyeshaje kwamba alijua kwamba Yesu alikuwa mtu muhimu?<br>• Aliuliza nini?<br>• Taja amri zozote ambazo Yesu alitaja.<br>• Kijana huyo alisema nini kuhusu amri hizi?<br>• Yesu alimwambia afanye nini ili kuonyesha kwamba Yesu alikuwa wa maana zaidi kuliko pesa zake?<br>• Je, alifaulu au alifeli mtihani? Kwa nini? |

## C4 Habari ya Kwanza

**Habari ya Pasaka –Habari hii inahusu Yesu kusalitiwa.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Yuda alimsaliti Yesu kwa vipande 30 vya fedha.<br>• Yesu aliwaruhusu adui zake wamkamate kwa sababu alijua kilicho mbele ni mpango wa Mungu kwetu.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mathayo 26: 24***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Mathayo 26: 14-16 & 36-50*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Waulize watoto kama wanakumbuka miujiza aliyoifanya Yesu au kama wanaweza kutaja watu aliowasaidia katika C2. Je, wanaweza kukumbuka watu aliokutana nao na kuzungumza nao katika C3? Ni mambo gani makuu ambayo Yesu alizungumzia? (uzima wa milele/ msamaha) Ongoza kusema kwamba sababu ya Yesu kuja ilikuwa kubwa kuliko uponyaji au mafundisho. Ilikuwa ni kutekeleza mpango wa Baba yake kufa msalabani ili tuweze kusamehewa dhambi zetu na kuwa na uzima wa milele. |
| **FUNDISHA** | • Makuhani wakuu na wazee wa watu walipanga njama kutafuta njia ya kumuua Yesu. Yuda, mmoja wa wanafunzi wa Yesu, aliwaendea na kuwaahidi kuwaongoza kwa Yesu. Wakamlipa vipande 30 vya fedha. Yuda 'alimsaliti' Yesu. *Eleza maana ya neno 'kusalitiwa'. Jadili ukweli kwamba Yuda alimsaliti Yesu kwa sababu alitaka pesa zaidi kuliko alivyotaka kumfuata Yesu. Hakumpenda Yesu na hakuwa mfuasi wa kweli.* ***(Mathayo 26: 14-16)***<br>• Jioni moja, Yesu alienda na wanafunzi Wake wote, isipokuwa Yuda, kwenye bustani ya Gethsemane. Katika bustani, Yesu alimwomba Petro, Yakobo, na Yohana wamngojee na kukesha huku akienda peke yake kusali kwa Baba yake, Mungu. Yesu alijua kile ambacho kilikuwa karibu kutokea. Biblia inatuambia kwamba alianza ''kuhuzunika na kusononeka'. *Kwa nini Yesu alihisi hivyo?* Ingawa alijua kitakachotokea, aliomba, 'Si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe'. *Eleza kwamba Yesu alikuwa tayari kutekeleza mpango wa Mungu na kujiachia asulubiwe kwa sababu alitupenda na alitaka kuchukua adhabu kwa ajili ya dhambi zetu.* ***(Mathayo 26: 36-39)***<br>• Yesu alipokuwa akiomba, wanafunzi walilala. Jambo hili lilifanyika mara tatu, na kila mara Yesu alikuja na kuwaamsha. Baada ya hapo, Yesu alijua kwamba wakati ulikuwa umefika wa Mapenzi ya Mungu kutimizwa. ***(Mathayo 26: 40-46)***<br>• *Eleza ukimya uliovunjwa na nyayo zikitembea gizani.* Alikuwa ni Yuda, pamoja na umati wa watu waliokuwa wamebeba panga na marungu. *Unafikiri wangefanya nini?* Eleza kwamba hawakuweza kutofautisha nyuso kwa urahisi gizani, lakini Yuda alimjua Yesu na akaenda Kwake na kumbusu. Hilo liliwafanya wajue wangemkamata nani, na Yesu akawaruhusu watu hao wamkamate. Kisha akawaruhusu wale watu wamkamate. ***(Mathayo 26: 47-50)***<br>• Yuda alikuwa amefanya kosa kubwa sana kwa kumsaliti Yesu. *Bila kutoa mifano ya kibinafsi, zungumza na watoto kuhusu jinsi ilivyo vibaya kukatishwa tamaa na mtu ambaye tulifikiri tunaweza kumwamini.* Yuda alitaka pesa kuliko alivyotaka kumfuata Yesu.<br>• Yesu anatupenda sana kiasi kwamba alikuwa tayari kuteseka sana alipokuwa akiomba katika bustani na kusalitiwa na rafiki wa uongo. Yote ilikuwa ni sehemu ya kile alichopaswa kupitia ili kutekeleza mpango wa Mungu kwa ajili yetu. Baadaye, Yesu angebeba adhabu yote kwa ajili ya dhambi zetu.<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B: Yesu asalitiwa. |
| **JIFUNZE** | Inapofaa, fundisha na elezea Mstari Muhimu – ***Mathayo 26: 24***. Watoto wa Daraja la kwanza wanaweza kujifunza nusu ya kwanza ya mstari. |
| **KUMBUKA** | Tumia maswali haya kwa jaribio:<br>• Ni nani waliopanga pamoja kumuua Yesu?<br>• Mwanafunzi aliyemsaliti Yesu aliitwa nani?<br>• Neno 'kusalitiwa' lina maana gani?<br>• Walimlipa Yuda vipande vingapi vya fedha?<br>• Je, bustani ambayo Yesu alienda kusali iliitwa nini?<br>• Ni nini kiliwapata wanafunzi Yesu alipokuwa akisali?<br>• Yuda aliwaonyeshaje watu kuwa Yesu alikuwa yupi?<br>• Kwa nini Yesu aliruhusu Mwenyewe kukamatwa? |

## C4 Habari ya Pili

**Habari ya Pasaka– Habari hii inahusu Yesu kuteseka kwa ajili yetu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Yesu hakuwa na hatia.<br>• Yesu alikufa kwa sababu ya dhambi zetu.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mathayo 27: 22***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Mathayo 27: 1-2 & 11-31*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Rejea habari iliyotangulia pamoja na watoto. Yesu alikuwa amekamatwa na umati uliotumwa na viongozi wa Kiyahudi. Waulize watoto kama wamewahi kupata matatizo kwa jambo ambalo hawakufanya. Labda waliadhibiwa wakati hawakufanya kosa lolote. Je, hii ilikuwa haki? Je, hali hii iliwafanya wajisikie vipi? Katika habari ya leo jaribu kufikiria jinsi ilivyokuwa kwa Yesu, Mwana wa Mungu asiye na dhambi, kushtakiwa kwamba amefanya makosa. |
| **FUNDISHA** | • Yesu alifungwa na kupelekwa kwa Pilato, Liwali wa Kirumi. *Eleza kwamba viongozi wa Kiyahudi walipaswa kumpeleka Yesu kwa Pilato kwa sababu alikuwa msimamizi wa nchi yao wakati huo.* ***(Mathayo 27:1-2)***<br>• Pilato alimuuliza Yesu maswali. Alihisi hakika kwamba Yesu hakuwa na hatia. *Wakumbushe watoto kwamba Yesu hakuwahi kufanya dhambi yoyote.* Hakuwa na dhambi. Pilato alijua kwamba viongozi wa Kiyahudi walitaka Yesu asulibiwe kwa sababu walimwonea wivu. Walisema uwongo mwingi kuhusu Yesu. Pilato hakutaka kumtoa Yesu asulubiwe hivyo alijitolea kumfungua mfungwa mmoja. Aliona kwamba Wayahudi wanaweza kuchagua mtu ambaye angewekwa huru. Pilato alitumaini wangemchagua Yesu, lakini hawakumchagua. Wakamchagua Baraba ambaye alikuwa mtu mwovu na wakapiga kelele kwamba Yesu asulibiwe. *Uliza, 'Je, Yesu alistahili kusulubiwa? Unafikiri jambo hilo lilikuwa sawa?' Zungumzia kwa nini Mungu aliruhusu Yesu atendewe hivyo.* ***(Mathayo 27:11-23)***<br>• Pilato alijua kwamba watu hawangebadili mawazo yao. Alimfungua Baraba na kuamuru kwamba Bwana Yesu apigwe mijeledi na kuchukuliwa asulubiwe kwenye msalaba. Kabla hawajamsulubisha, askari walimtendea vibaya sana. Walimvika vazi la rangi nyekundu na kumvika taji ya miiba kichwani. Wakamdhihaki, wakamtemea mate, na kumpiga. Kisha wakamsulubisha kwa kumpigilia misumari msalabani. ***(Mathayo 27: 24-31)***<br>• **Daraja la 2** - *Unaweza kuchunguza zaidi kwa nini Yesu alikufa. Haikuwa haki kwamba mtu mbaya kama Baraba aachiwe na Yesu ambaye hakufanya kosa lolote auawe. Eleza kwamba Mungu alikuwa bado anatawala ingawa ilionekana kuwa watu walikuwa na uwezo juu ya kile kilichokuwa kikitokea kwa Yesu. Yesu alikuwa amewaeleza wanafunzi wake mapema kwamba angekufa kwa namna hii ingawa hawakuwa wameelewa.* ***(Mathayo 16: 21, 17: 22-23, 20: 17-19)*** *Manabii katika Agano la Kale pia walikuwa wameandika kuhusu matukio haya kabla hayajatukia. Sasa yote yalikuwa yanatendeka kama Mungu alivyopanga.*<br>• **Daraja la 1 na 2** - *Yesu hakustahili kufa. Alikufa kwa hiari kwa sababu alitupenda na alitaka kuchukua adhabu ya dhambi zetu. Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu wote. Lilikuwa tukio kubwa zaidi katika historia, lakini tunahitaji kufanya jambo kuhusu hilo kibinafsi. Tunapomwambia Yesu kwamba tunajutia dhambi zetu, atatusamehe na kuchukua dhambi zetu. Kisha tunaweza kuwa na uhakika kwamba siku moja tutakuwa pamoja Naye Mbinguni.*<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Habari ya Pasaka: Yesu kuteseka kwa ajili yetu (Pilato). |
| **JIFUNZE** | Fundisha na ueleze inapofaa Mstari Muhimu ambao ni sehemu ya habari – ***Mathayo 27: 22.*** |
| **KUMBUKA** | **Tumia taarifa hizi za Kweli/Si Kweli kwa ajili ya jaribio:**<br>• Pilato alimuuliza Yesu maswali.<br>• Pilato alidhani kwamba Yesu alikuwa na hatia.<br>• Viongozi wa Kiyahudi hawakutaka Yesu asulibiwe.<br>• Yesu hakuwahi kufanya dhambi yoyote.<br>• Baraba hakuwa na hatia.<br>• Askari walimtendea Yesu kwa wema.<br>• Yesu alichukua adhabu ambayo dhambi zetu zinastahili.<br>• Tunaweza kuwa Mbinguni pamoja na Yesu ikiwa tumesamehewa dhambi zetu. |

## C4 Habari ya Tatu

**Habari ya Pasaka – Habari hii inahusu Yesu kufufuka kutoka kwa wafu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Yesu alizikwa na kufufuka tena.<br>• Nguvu kuu za Mungu zilimfufua Yesu kutoka kwa wafu.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mathayo 28: 6***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Mathayo 27: 57-66*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Pitia masomo mawili yaliyotangulia. Watoto wanapotaja kile kilichotokea kwa Yesu, weka maneno haya kwenye vipande vya kadi vyenye alama rahisi ya picha, au uandike ubaoni kama inavyopendekezwa.<br>**kusalitiwa kukamatwa kuhojiwa kuhukumiwa kudhihakiwa kusulubiwa.**<br>Je, wanaweza kuyaweka katika mpangilio sahihi? Zingatia tena kwa nini haya yote yalitokea. |
| **FUNDISHA** | • Yesu alikufa msalabani. Jioni hiyohiyo, tajiri mmoja aitwaye Yusufu, alikwenda kuzungumza na Pilato. Yusufu alimwamini Yesu na alimwomba Pilato kama angeweza kuuchukua mwili wa Yesu ili akauzike inavyopasa. ***(Mathayo 27: 57-58)***<br>• Yusufu aliutwaa mwili, akaufunga katika sanda safi ya kitani, na kuuweka katika kaburi lake jipya. Kaburi hilo lilikuwa kama pango dogo lililochongwa kwenye mwamba. Alivingirisha jiwe kubwa mlangoni na kuondoka. Baadhi ya wanawake waliomfuata Yesu walibaki kaburini. *Waulize watoto wanafikiri Yusufu na wanawake hawa walikuwa wakihisi nini.* ***(Mathayo 27: 59-61)***<br>• *Waelezee watoto kwamba miaka mingi kabla ya tukio hili nabii Isaya alikuwa ametabiri kwamba Yesu angezikwa katika kaburi la tajiri* ***(Isaya 53: 9)****. Unabii huu sasa ulikuwa umetimia.*<br>• Wayahudi walikuwa na wasiwasi kwamba wanafunzi wa Yesu wanaweza kuja usiku, kuiba mwili Wake na kutunga habari kwamba Yesu alikuwa amefufuka kutoka kwa wafu. Walimwomba Pilato kama angeweza kutuma askari fulani kwenda kulifunga kaburi na kulilinda. ***(Mathayo 27: 62-66)***<br>• Askari walilinda kaburi, lakini hawakuweza kumzuia malaika wa Bwana kushuka kutoka Mbinguni. Akavingirisha lile jiwe na kulikalia. Yesu hakuwa kaburini tena! Malaika akasema, 'Hayupo hapa, kwani amefufuka kama alivyosema.' ***(Mathayo 28: 1-6)***<br>• Habari njema ni kwamba Mungu, kwa uwezo wake mkuu, alimfufua Bwana Yesu kutoka kwa wafu. Mwili wake haukuibiwa. Haukuoza. Mungu alimtoa kaburini akiwa hai! Hii inathibitisha jinsi Mungu alivyofurahishwa na kile Bwana Yesu alichokuwa amekifanya, alipokufa kwa ajili ya dhambi zetu. *Wakumbushe watoto kwamba inathibitisha pia kwamba Yeye kweli ni Mwana wa Mungu. Anataka kila mtu amtumainie kama Mwokozi wake mwenyewe.*<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Habari ya Pasaka: Yesu kufufuka kutoka kwa wafu (Yusufu wa Arimathaya). |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa fundisha na ueleze Mstari Muhimu, ambao ni sehemu ya habari – ***Mathayo 28: 6***. |
| **KUMBUKA** | Shughuli ya Sanaa ya Pasaka<br>Gawa darasa katika makundi matatu. Kila kikundi kinapewa muhtasari rahisi wa tukio.<br>1) Misalaba mitatu.<br>2) Kaburi lililo na jiwe mlangoni.<br>3) Kaburi ambalo jiwe limevingirishwa.<br>Kwa kutumia mabaki ya karatasi/nyenzo n.k. kikundi kinaweza kuunda kolagi. Maelezo/mstari unaweza kuongezwa unapoonyeshwa ***(1 Wakorintho 15: 3-4)***. Kikundi kidogo kinaweza kuzingatia onyesho la tatu. |

<u>C4 Habari ya Nne</u>

**Habari ya Pasaka — Habari hii inahusu Yesu kuwatokea wafuasi Wake.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Yote yaliyompata Yesu yalikuwa ni mpango wa Mungu.<br>• Kufufuka kwake kunaleta furaha kubwa.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 24: 26***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Luka 24: 13-35*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Pitia Shughuli: Fikiri, Oanisha, Shirikisha.<br>Tengeneza seti ya kadi ndogo zenye jina moja lililoandikwa kwa kila moja - Yuda, Pilato, Yusufu, wanawake. Utahitaji za kutosha kugawia moja kati ya wawili.<br>Wakifanya kazi wawiliwawili, watoto huelezana ni **nani, nini** na **wapi** wahusika wanafaa katika habari hii. Mwalimu anaweza kuchagua baadhi ya vikundi vya wawiliwawili ili kushirikisha kwa wanakikundi wengine mwishoni. |
| **FUNDISHA** | • Wafuasi wawili wa Yesu (mmoja aliitwa Kleopa) walikuwa wakitembea kutoka Yerusalemu kwenda kwenye kijiji kiitwacho Emau, umbali wa maili 7. Walikuwa wakizungumza kuhusu mambo yote yaliyotukia Yerusalemu na kuhuzunika sana na kuchanganyikiwa. *Jadili kwa nini. Eleza kwamba Yesu alikuwa amefufuliwa kutoka kwa wafu, lakini wafuasi hawa walikuwa bado hawajamwona.* ***(Luka 24: 13-14)***<br>• Mara mgeni alijiunga nao na kutaka kujua walichokuwa wakizungumza. *Eleza kwamba wewe utakuwa Kleopa ukizungumza na mgeni. Onyesha huzuni na kuchanganyikiwa:*<br>• Je, hujasikia kuhusu kile ambacho kimetokea Yerusalemu? Utakuwa ni wewe tu hujasikia habari hii! Yesu wa Nazareti alikuwa nabii kutoka kwa Mungu na pia tulitumaini kwamba angekuwa mkombozi maalum kutoka kwa Mungu. Alisema na kufanya mambo mengi ya ajabu. Lakini siku tatu zilizopita, viongozi wetu walimwua msalabani. Leo wanawake walituambia habari za kushangaza. Mapema asubuhi ya leo, walitembelea kaburi alimokuwa amezikwa lakini hawakuweza kuupata mwili Wake. Walituambia kwamba kulikuwa na malaika ambao walisema kwamba Yesu yu hai! Kisha baadhi ya marafiki zetu wengine walikwenda kaburini na kukuta kaburi likiwa tupu, sawa na vile wanawake walivyosema, lakini hapakuwa na alama yoyote ya Yesu! ***(Luka 24: 15-24)***<br>• *Nyamaza kidogo... na ueleze kwamba sasa utasema jibu la mgeni...* Wewe hufahamu na mzito kiasi gani kutambua ukweli! Unatakiwa kuamini kila kitu ambacho manabii walisema na kile kilichoandikwa katika Maandiko. Aliyetumwa na Mungu alipaswa kuteseka.<br>• *Mgeni alieleza jinsi yote ambayo Mungu aliwaambia manabii wa Agano la Kale yalivyotimia. Wafuasi wawili wa Yesu walishangaa jinsi mgeni huyo alivyojua yote hayo!* ***(Luka 24: 25-27)***<br>• Punde, wote watatu walifika Emau. Kulikuwa kumekuchwa, hivyo wakamsihi yule mgeni abaki na kulala usiku huo. Walipokuwa wakila, yule mgeni akachukua mkate, akaumega na kumshukuru Mungu. *Je, hiyo inakupa fununu kuhusu mgeni huyo alikuwa nani?* Biblia inasema macho yao yakafumbuliwa wakajua ni Yesu! Ghafla alitoweka asionekane, lakini sasa walikuwa na hakika kabisa kwamba Yesu alikuwa amefufuka kutoka kwa wafu! Walitambua jinsi ilivyokuwa vizuri kumsikia akieleza yote kuhusu Yeye mwenyewe walipokuwa njiani.<br>• *Linganisha shangwe na mshangao walionao sasa ikilinganishwa na hapo awali.* ***(Luka 24: 28-32)***<br>• Mara walirudi Yerusalemu na kuwakuta wanafunzi. Waliwaambia kuhusu mazungumzo ya barabarani na jinsi yalivyowafikisha katika kumgundua Yesu. ***(Luka 24: 33-35)***<br>• *Katika habari hii, wafuasi wawili walijifunza kutoka kwa Yesu kuhusu mpango wa Mungu na jinsi yote yalivyofanyika. Sisi pia tunapaswa kufurahi kwamba tunaelewa kutoka katika Biblia kuhusu Yesu akitayarisha njia ya kuturudisha kwa Mungu. Ilimpasa kuteseka na kufa ili kuchukua adhabu ya dhambi zetu. Pia ulikuwa ni mpango wa Mungu kwamba angefufuka tena na kurudi Mbinguni. Biblia inatufundisha kwamba tunapaswa kumshukuru kwa yote ambayo ametufanyia ili dhambi zetu zisamehewe, na tutazamie kwa hamu kuwa pamoja naye Mbinguni.*<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Habari ya Pasaka: Yesu kuwatokea wafuasi wake. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na ueleze Mstari Muhimu ambao ni sehemu ya habari – ***Luka 24: 26***. |
| **KUMBUKA** | Shughuli ya kikundi: Andaa hadithi kwa kila kikundi ili kuzifanya sentensi zilizochanganyika ziwe katika mpangilio. Kundi la kwanza kufanya hivyo kwa usahihi ndio watakuwa ni washindi. Hapa kuna sentensi. Wafuasi wawili wa Yesu walikuwa wakienda Emau - Walikuwa na huzuni - Mgeni alijiunga nao -Mgeni alizungumza kuhusu kilichotokea - Huko Emau, mgeni alijiunga nao kula chakula - Walijua ni Yesu alipomega mkate - Walijawa na furaha kwa sababu Yesu alikuwa hai.<br>**Watoto wa Daraja la 1** wanaweza kuchora picha za watu hao barabarani au wakila chakula pamoja walipofika Emau. |

## C5 Habari ya Kwanza

**Ruthu – Habari hii inahusu kumtumaini Mungu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Ruthu alimwamini Mungu alipofanya uamuzi wa kurudi Bethlehemu.<br>• Mungu anataka tumtumaini Yeye.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Ruthu 1: 16-17***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Ruthu 1*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Zungumza kuhusu jinsi tunavyofanya maamuzi mengi kila siku, ukirejelea mifano. Kulingana na kikundi, unaweza kumpa kila mtu fursa ya kufanya chaguo k.m., kati ya shughuli/michezo miwili ya kufanya baadaye au kati ya zawadi ndogo mbili.<br>Habari ya leo inajumuisha watu tofauti ambao walifanya maamuzi. Changamoto kwa watoto kusikiliza kwa makini na kuhesabu maamuzi yote kama yalivyotajwa. Mmoja wa watu katika habari alifanya uamuzi ambao ulibadilisha maisha yake yote! |
| **FUNDISHA** | • Kulikuwa na njaa *(eleza hii ina maana gani)* huko Bethlehemu. Mwanaume aliyeitwa Elimeleki aliamua kuwa ni afadhali kumchukua mkewe Naomi na wanawe wawili hadi nchi nyingine iitwayo Moabu. ***(Ruthu 1: 1-2)***<br>• La kusikitisha, Elimeleki alikufa. Wanawe wawili walikua ambapo kila mmoja wao aliamua kuoa msichana kutoka Moabu. Baada ya muda mfupi, wale vijana wawili walikufa! *(Daraja la 2 – taja majina yao)* Sasa walibaki tu Naomi na wale wanawake vijana wawili, Orpa na Ruthu. *Jadili kwa umakini jinsi watatu hao walivyojisikia.* ***(Ruthu 1: 3-5)***<br>• Punde Naomi aliamua kurudi katika mji wake mwenyewe wa Bethlehemu. Alianza safari pamoja na Orpa na Ruthu ambao walitaka kwenda naye pia. Baada ya kutembea kidogo, Naomi aliwaambia ingekuwa afadhali kama wangebaki Moabu, nchi yao wenyewe. Orpa aliamua kurudi nyumbani. Hata hivyo, Ruthu hakubadili mawazo yake. *Jadili jinsi huu ulivyokuwa uamuzi wa "ujasiri" kwa Ruthu; alitarajiwa kuwa mgeni katika Bethlehemu na hangejua jinsi ambavyo maisha yangekuwa huko. Soma maneno yake katika* ***Ruthu 1: 16-17*** *na ueleze jinsi ulivyokuwa uamuzi wake wa kukubali maisha mapya kati ya watu tofauti lakini muhimu zaidi kumwamini Mungu aliye hai na wa kweli ambaye alikuwa amejifunza habari zake kupitia kwa Naomi.* ***(Ruthu 1: 5-16)***<br>• *Eleza kwamba Mungu anataka tujifunze kutokana na mfano wa Ruthu. Alituumba na anajua ni nini kilicho bora kwetu. Anatutaka tumwamini na kumpa nafasi atimize mpango wake kwa ajili ya maisha yetu.*<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho C – Ruthu. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa jifunze na ueleze Mstari Muhimu – ***Ruthu 1: 16***. Fupisha mstari, inapobidi. |
| **KUMBUKA** | Tumia maswali haya kwa ajili ya jaribio:<br>1. Kwa nini Elimeleki alichagua kuondoka Bethlehemu?<br>2. Alikuwa na wana wangapi?<br>3. Ni wanawake wangapi walipanga kurudi Bethlehemu?<br>4. Ni nani aligeuka kurudi Moabu?<br>5. Nani aliendelea na safari pamoja na Naomi?<br>6. Ni sehemu gani iliyo bora zaidi ya uamuzi wa Ruthu?<br>7. Ni jambo gani lingekuwa gumu kuhusu uamuzi wa Ruthu?<br>8. Swali la changamoto: Ni maamuzi mangapi yametajwa kwenye habari? (7) Watoto wanaweza kukumbuka yalikuwa yapi. |

## <u>C5 Habari ya Pili</u>
**Ruthu na Boazi – Habari hii inahusu mpango wa Mungu kuhusu Ruthu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Mungu alikuwa mwema kwa Ruthu na akatimiza mpango Wake kwa maisha yake.<br>• Mungu ana mpango kwa ajili ya maisha yetu.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Ruthu 4: 13***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Ruthu 2-4*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Pitia mambo muhimu ya habari ya wiki iliyopita. Zungumza kuhusu wakati wa mavuno. Je, unaweza kutaja baadhi ya mazao? Onyesha baadhi ya picha/mifano. Zungumza jinsi yanavyovunwa. Katika nyakati za Biblia, hapakuwa na mashine. Wavunaji walitumia visu vikubwa vinavyoitwa mundu kukata nafaka. Watu maskini walioitwa waokota masazo waliruhusiwa kufuata nyuma ya wavunaji na kuchukua masuke yoyote ya nafaka ambayo yalikuwa yamebaki. |
| **FUNDISHA** | • Ruthu na Naomi walipofika Bethlehemu ilikuwa ni wakati wa mavuno ya shayiri. Ruthu alitaka kufanya kazi ya kuokota masazo ili kutoa huduma ya chakula kwa ajili ya Naomi na yeye mwenyewe. *Jadili hii kazi ilikuwaje? (kazi ngumu, bila kumjua mtu yeyote)* Huenda Ruthu alishangaa wakati mwenye shamba, mtu anayeitwa Boazi, alipomtendea kwa wema sana. Akamwambia akae shambani kwake pamoja na vijakazi wake na kunywa maji atakapoona kiu. ***(Ruthu 2: 8-9)***<br>• Ruthu alishangaa kwa nini alimtendea kwa wema hivyo mtu ambaye ni mgeni, lakini Boazi akaeleza kwamba tayari alikuwa amesikia habari zake! *Waombe watoto wajaribu kutafuta kile ambacho inawezekana alisikia kuhusu Ruthu.* Boazi alijua kwamba Ruthu alikuwa akimtumaini Mungu. Mungu alikuwa akimtumia Boazi kumtunza Ruthu. ***(Ruthu 2: 10-17)*** Baadaye, Boazi alimwandalia Ruthu chakula cha mchana na pia akawaambia wanaume hao wahakikishe wamemwachia nafaka ya ziada ili aokote.<br>• *Waulize watoto kile ambacho Ruthu angemwambia Naomi aliporudi nyumbani jioni ile. Eleza kwamba Naomi alijua kwamba matendo yote ya Boazi yalikuwa ni fadhili za Mungu kwa Ruthu.* ***(Ruthu 2: 18-23)***<br>• *Toa muhtasari wa mwisho wa habari* ***(Ruthu 3 na 4)*** *kwa kueleza kwamba Mungu alikuwa na mipango mizuri zaidi kwa maisha ya Ruthu.* Baada ya muda mfupi yeye na Boazi wakaoana. Baadaye, Ruthu alipata mtoto wa kiume anayeitwa Obedi. *Eleza kwamba alikuwa babu wa Mfalme Daudi. Zungumza jinsi matukio haya ya furaha yalivyowaathiri Ruthu na Naomi - linganisha na wakati uliopita. Wasaidie watoto kuona kwamba uamuzi wa Ruthu wa kumchagua Mungu katika* ***Ruthu 1: 16*** *ulikuwa sahihi. Eleza kwamba tunapomtumaini Mungu, Mungu ataleta mpango Wake mzuri na mkamilifu kwa ajili yetu.*<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho C – Ruthu na Boazi. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa jifunze na ueleze Mstari Muhimu – ***Warumi 8: 28***. Mungu alitumia uchaguzi ambao Ruthu alifanya na hata mambo magumu yaliyompata (akiwa mgeni katika nchi nyingine) ili mpango Wake mzuri kwa ajili yake utimie. |
| **KUMBUKA** | **Daraja la 1** - Hizi hapa ni baadhi ya taarifa za msingi za kukumbuka za Kweli/Si Kweli kuhusu habari:<br>1. Naomi na Ruthu walifika majira ya kuchipua.<br>2. Wote wawili walipata kazi ya kufanya mashambani.<br>3. Ruthu alifanya kazi katika shamba la Boazi.<br>4. Boazi alimtunza Ruthu kwa kuhakikisha ana chakula na maji.<br>5. Naomi hakuelewa kwa nini Boazi alikuwa akimtendea wema Ruthu.<br>6. Baadaye Boazi alimwoa Ruthu na wakapata mtoto wa kiume.<br><br>**Daraja la 2** - Unaweza kujadili kauli hizi:<br>1. Ruthu alikuwa na wakati mgumu alipokuja Bethlehemu pamoja na Naomi.<br>2. Mambo mazuri yalimtokea kwa bahati.<br>3. Mungu hutumia watu wengine kufanya mipango yake kwa ajili ya maisha yetu. (Zingatia ushawishi wa Naomi na Boazi katika maisha ya Ruthu) |

## C5 Habari ya Tatu

**Hana amuomba Mungu – Habari hii inahusu jinsi Mungu anavyosikia maombi yetu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Mungu alisikia na kujibu maombi ya Hana.<br>• Mungu anataka tuombe.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 11: 9***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***1 Samweli 1: 1-20*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Zungumza kuhusu maombi. Watoto watakuwa na viwango tofauti vya kuelewa maombi ni nini. Jaribu kuwaondoa katika mtazamo kwamba maombi ni aina fulani ya orodha ya matamanio. Badala yake, Mungu ni Baba yetu wa Mbinguni na anataka kutupa kile Anachojua ni bora kwetu. Eleza ajabu ya kuweza kuzungumza na Mungu, ukijua anasikiliza. Kwa Daraja la 2, unaweza kuangalia baadhi ya vitu sahihi vilivyotajwa kwenye orodha ya maombi. |
| **FUNDISHA** | • Eleza hali ambayo Hana alijikuta akipitia. *(aya ya kwanza ya somo la Daraja la 2)* ***(1 Samweli 1: 1-2)***<br>• Kila mwaka Elkana aliendа na familia yake kwenye safari ya pekee hadi mahali paitwapo Shilo. Hapa wangeweza kumwabudu Mungu. Lakini wakati huu, Hana alikasirika sana kwa sababu Penina alikuwa amezungumza naye kwa uchungu kuhusu kutokuwa na mtoto. Alikuwa akilia na hakutaka kula. Hana alifanya jambo bora zaidi aliloweza. Aliamua kumwomba Mungu. *Eleza kwamba tunaweza kuzungumza na Mungu kuhusu mahangaiko na matatizo yetu.* ***(1 Samweli 1: 3-7)***<br>• Hana alipokuwa akisali, aliweka ahadi kwa Mungu. Kama angempa mtoto wa kiume, angemrudisha kwa Mungu ili amtumikie. Mtu mwingine alikuwa akitazama! Kuhani Eli, aliona kwamba Hana alikuwa akilia lakini alipotazama midomo yake ikinena, hakuweza kusikia neno lolote. Eli alifikiri kwamba alikuwa amelewa, hivyo akamsema! Hana alimweleza Eli kwamba alikuwa na huzuni sana, na alikuwa akiomba kwa Bwana. *Zungumza kuhusu jinsi tunavyoweza kuomba kutoka mioyoni mwetu kama Hana. Hatuhitaji hata kusema kwa sauti. Mungu anajua tunamaanisha nini hasa katika maombi yetu.* ***(1 Samweli 1: 9-16)***<br>• Kisha Eli akamwambia Hana, “Nenda nyumbani kwako, wala usifadhaike, na Mungu akupe ulichomwomba.” *Waambie watoto watabiri jinsi Hana alivyokuwa akijisikia sasa na kuzungumza kuhusu tofauti inayotokea tunapokabidhi matatizo yetu kwa Mungu.* ***(1 Samweli 1: 17-18)***<br>• Wakati fulani baadaye Mungu alijibu maombi ya Hana. Alikuwa na mtoto wa kiume. Alimwita Samweli jina lenye maana ya "kuombwa kwa Mungu". Hana hakusahau kwamba mtoto Samweli alikuwa jibu la sala yake. ***(1 Samweli 1: 19-20)*** *Tunapaswa kukumbuka daima kumshukuru Mungu kwa kujibu maombi yetu.*<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho C – Hana amwomba Mungu. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa jifunze na ueleze Mstari Muhimu – ***“Ombeni nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtapata.”*** Eleza kwamba maneno haya yalisemwa na Yesu. Anataka kutubariki. Zaidi ya yote, anataka kutupa zawadi ya wokovu kwa kutuokoa kutoka kwenye dhambi zetu. |
| **KUMBUKA** | Tumia maswali haya kwa ajili ya jaribio:<br>• Elkana aliipeleka wapi familia yake kila mwaka?<br>• Kwa nini Hana alikasirika sana?<br>• Hana hakutaka kufanya nini?<br>• Kuhani Eli aliona nini kuhusu Hana alipokuwa akisali?<br>• Hana aliweka ahadi gani?<br>• Hana alijisikiaje baada ya kuomba?<br>• Alimwitaje mtoto wake wa kiume?<br>• Jina la mtoto wake lilikuwa na maana gani? |

## C5 Habari ya Nne

**Samweli asikia wito wa Mungu – Habari hii inahusu Mungu kusema na Samweli.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Samweli aliitika Mungu alipomwita.<br>• Kila mmoja wetu anahitaji kumwitika Bwana kibinafsi.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***1 Samweli 3: 9***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***1 Samweli 1: 21-3: 21*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Cheza mchezo rahisi wa "Simu na Mwitikio" pamoja na watoto. Kiongozi anatumia ngoma/kupiga makofi kufanya mabadiliko kwenye mdundo wa 4/4 na kikundi cha watoto kinarudia. Watoto wanaweza kubadilishana kuwa kiongozi. Kuna mawazo mengi ya "Simu na Mwitikio" kwa kutumia maneno au kauli mbiu k.m. kiongozi anamwita L. I. S. na watoto kuitikia T.E.N! |
| **FUNDISHA** | • *Rudia ahadi iliyotolewa na Hana katika somo la wiki iliyopita. Eleza kwamba Samweli alipokuwa angali mvulana mdogo, Hana alitimiza ahadi yake.* Alimpeleka Samweli Shilo. Pia, Hana akamwomba Mungu; wakati huu aliomba sala ya furaha kuhusu yote ambayo Mungu alimkusudia. ***(1 Samweli 1: 24-2: 11)***<br>• Samweli akiwa mdogo alianza kumtumikia Mungu. *Eleza kwamba Samweli alikuwa mtoto maalum mwenye kazi maalum.* Mungu alikuwa na mipango kwa ajili ya maisha ya Samweli. Hana hakusahau kuhusu Samweli. Kila mwaka alipomtembelea pamoja na familia yake, alimletea kanzu mpya. *Zungumza kuhusu wakati huu ulivyokuwa wa furaha kwao wote wawili.* Samweli alipokua, maisha yake yalimpendeza Mungu na watu wengine waliomjua. *Wape changamoto watoto unaowafundisha kujua kama maisha yao yanampendeza Mungu kadiri wanavyoendelea kukua.* ***(1 Samweli 2: 18, 21, 26)***<br>• Usiku mmoja baada ya Samweli kulala, alisikia mtu akimwita jina lake. Samweli alifikiri ni kuhani Eli na akamkimbilia. Lakini Eli alimwambia Samweli kwamba hakumwita na kumwambia arudi akalale. *Eleza jinsi hili lilivyotokea tena na uwasaidie watoto kufikiria jinsi Samweli alivyokuwa akihisi.* Samweli aliposikia jina lake likiitwa mara ya tatu, alienda tena kwa Eli, lakini wakati huu Eli alitambua ni nani aliyemwita Samweli. Alikuwa ni Mungu. Eli alimwambia Samweli kama angesikia jina lake likiitwa tena, angepaswa kujibu, "Nena Bwana, kwa kuwa mtumishi wako anasikia." ***(1 Samweli 3: 1-9)***<br>• Aliporudi kitandani, Samweli alisikia akiitwa mara ya nne. Samweli akamjibu Bwana kama Eli alivyomwambia. Hadi wakati huu wa maisha yake Samweli alijua kuhusu Bwana lakini hakumjua kibinafsi. Samweli alipojua kwamba Mungu anamwita, aliitikia kwa njia ifaayo. *Chora sambamba na mchezo wa utangulizi.* Usiku huo Mungu alimpa Samweli ujumbe muhimu kwa Eli. Huo ulikuwa ujumbe wa kwanza kati ya jumbe nyingi ambazo Samweli alipokea akiwa nabii kutoka kwa Mungu. ***(1 Samweli 3: 10-21)***<br>• Mungu alimjua Samweli kwa jina. Anamjua kila mmoja wetu kwa jina na anamwita kila mmoja wetu ampokee Mwanawe kama Bwana na Mwokozi wetu. *Eleza kwamba wito wa Mungu kwetu hausikiki kwa sauti kubwa bali kupitia kwa Roho Mtakatifu akitufahamisha kile tunachotakiwa kufanya. Mungu huzungumza nasi tunaposoma Biblia. Wape changamoto watoto kuhusu hitaji lao la kuitikia kwa njia sahihi.*<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho C – Samweli asikia wito wa Mungu. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa jifunze na ueleze Mstari Muhimu – ***1 Samweli 3: 9*** |
| **KUMBUKA** | Tumia maswali haya kwa ajili ya jaribio:<br>• Hana alimpeleka wapi Samweli kufanya kazi?<br>• Alimletea nini kila mwaka?<br>• Maisha ya Samweli yalimpendeza nani?<br>• Ni nani aliyefanya kazi na Samweli?<br>• Mungu alimwita Samweli mara ngapi?<br>• Samweli alipaswa kumjibuje Bwana alipomsikia akizungumza?<br>• Je, Mungu anajua majina yetu?<br>• Tunapaswa kufanya nini Mungu anapotuita? |

<u>**C6 Habari ya Kwanza**</u>

**Daudi – Habari hii inahusu Mungu kumchagua Daudi kuwa Mfalme.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Mungu alimwambia Samweli amchague Daudi kuwa mfalme wa Israeli.<br>• Mungu anapendezwa na jinsi tulivyo - si jinsi tunavyoonekana.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***1 Samweli 16: 7***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***1 Samweli 16: 1-13*** |
| **TOA UTANGULIZI** | (Katika habari nne zinazofuata kuna vipengele vilivyopendekezwa vilivyoandikwa kwa **kukolezwa wino** ili vionyeshwe vinapotajwa. Kisha vinatumiwa kwenye marudio mwishoni mwa Habari ya 4.)<br>Tuseme umetumwa kwenye misheni ya kuchagua mfalme mpya, ungechagua mtu wa aina gani? Panga majibu ya watoto katika seti 2 - zinazohusiana na mwonekano na sifa. Jadili yapi ni muhimu zaidi. Inaweza kuwa vigumu kujua mtu ni wa namna gani ikiwa hujawahi kukutana naye. Kwa kuwa na kielelezo, uwe na zawadi mbili zilizofungwa, zote mbili ziwe zinaonekana ni nzuri kwa nje. Chagua watoto wawili wa kuzifungua ili kugundua kuwa moja ni halisi lakini nyingine haifai. |
| **FUNDISHA** | • Samweli alitumwa na Mungu kwa kazi ya siri ya kumtafuta mfalme anayefuata wa Israeli. Samweli alikuwa amechaguliwa na Mungu kama nabii ili kuwaambia watu kile ambacho Mungu alitaka kuwaambia. Mungu hakupendezwa na mfalme wa kwanza wa Israeli, Sauli - kwa vile hakumtii Mungu. ***(1 Samweli 15: 11)*** Samweli alikasirishwa na Sauli lakini Mungu alimwambia asiwe na huzuni. Badala yake, alipaswa kupeleka chupa ya mafuta ya mzeituni kwa mtu aliyeitwa Yese huko Bethlehemu ambaye alikuwa na wana wanane. Soma maneno ya Mungu kwa Samweli. ***(1 Samweli 16: 1)***<br>• Samweli alikuwa na wasiwasi. Kama Mfalme Sauli angesikia kwamba mtu mwingine amechaguliwa kuwa mfalme, angekasirika na kujaribu kumuua Samweli. Mungu alimwambia Samweli amtafute Yese na wanawe na kumwabudu Mungu pamoja kabla ya kuchagua mfalme mpya. Samweli alitii. *Ikiwa tunampenda Mungu, tunapaswa kumtii pia na kufanya yale anayosema katika Biblia.* ***(1 Samweli 16: 2-3)***<br>• Samweli alipofika Bethlehemu, viongozi wa jiji waliogopa na wakauliza ikiwa amekuja kuleta habari mbaya. Samweli alieleza kwamba alikuwa amekuja kumwabudu Mungu pamoja na Yese na wanawe. Hakuwaambia amekuja kupata mfalme mpya. *Kwa nini hakufanya hivyo?* ***(1 Samweli 16: 4-5)***<br>• *Eleza kile kilichotokea katika* ***1 Samweli 16: 6-11,****, ukisisitiza kile ambacho Mungu anamwambia Samweli katika* ***mstari wa 7****. Haijalishi kwa Mungu jinsi mtu anavyoonekana kwa nje. Mungu anapendezwa na vile tulivyo. Anajua mawazo yetu juu yake na wengine wanaotuzunguka. Rejea tena kielelezo kilichotumiwa katika utangulizi.*<br>• Daudi alikuwa kijana mwenye afya njema ambaye alitumia muda mwingi wa siku zake kwenye hewa safi akichunga kondoo wa baba yake. **(onyesha)** *Tumia maneno ya Mungu kwa Samweli katika* ***mstari wa 12b****.* Samweli alimimina mafuta ya mzeituni juu ya kichwa cha Daudi kama ishara kwamba siku moja angekuwa mfalme! Mungu alikuwa pamoja na Daudi tangu siku hiyo. Mungu alijua yaliyokuwa moyoni mwa Daudi Ingawa alikuwa mdogo zaidi kati ya wana wa Yese, alichaguliwa kuwa mtu anayefaa kuwa mfalme mwingine wa Israeli. *Eleza kwamba Mungu anajua jinsi kila mmoja wetu alivyo pia. Mungu haangalii urefu wetu, rangi ya nywele, au kama sisi ni wazuri. Anapendezwa na tunavyompenda Yeye na Mwanawe, Bwana Yesu.* ***(1 Samweli 16: 12-13)***<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho C – Kuchagua mfalme. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa fundisha na eleza Mstari Muhimu – ***1 Samweli 16: 7***. Chagua sehemu ya mwisho katika kuwafundisha watoto wadogo. |
| **KUMBUKA** | Unganisha vifaa vya kuona. Watoto waweke katika mpangilio sahihi na wasimulie habari tena. Semeni Mstari Muhimu kwa pamoja, au fanyeni jaribio:<br>• Ni nani aliyekuwa mfalme wa kwanza wa Israeli?<br>• Mungu alimchagua nani kupata mfalme mpya?<br>• Alienda wapi?<br>• Alilazimika kwenda akiwa amechukua nini?<br>• Kwa nini Samweli alikuwa na wasiwasi?<br>• Samweli aliambiwa amtafute nani huko Bethlehemu?<br>• Yese alikuwa na wana wangapi?<br>• Ni nani aliyekuwa mwana wa mwisho aliyeletwa kwa Samweli?<br>• Samweli alionyeshaje kwamba siku moja Daudi angekuwa mfalme mpya?<br>• Mungu anapendezwa zaidi na nini kuhusu sisi? |

## C6 Habari ya Pili
**Daudi – Habari hii inahusu Daudi kukabiliana na changamoto.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Daudi alijua Mungu angempa ushindi.<br>• Tunaweza kuwa na ujasiri mkuu katika Mungu aliye hai.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***1 Samweli 17: 26***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***1 Samweli 17: 1-31*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Je, umeshiriki katika changamoto zozote - matembezi yaliyofadhiliwa/kuogelea/kunyamaza ili kutafuta pesa kwa ajili ya shule yako au shirika la hisani? *Jadili.* Katika habari ya leo, jeshi la Israeli lilikuwa linakabiliwa na changamoto ngumu – jitu shujaa.<br>Kata m3 (futi 9 inchi 6) kutoka kwenye safu ya karatasi na kuiweka kwenye sakafu. Waambie watoto wajipime wenyewe dhidi ya urefu huo - urefu wa Goliathi. |
| **FUNDISHA** | • Israeli na Mfalme Sauli walikuwa kwenye vita na Wafilisti. *Wakumbushe watoto kwamba Waisraeli walikuwa watu wa pekee kwa Mungu na mara nyingi zamani alikuwa amelisaidia jeshi kushinda vita walipomtumaini Yeye. Eleza tukio la jeshi la Waisraeli upande mmoja wa bonde na Wafilisti upande mwingine.* Wafilisti hawakumpenda wala kumwamini Mungu. Badala ya majeshi yote mawili kupigana, Wafilisti walimtuma askari-jeshi wao shujaa, Goliathi, ili kulipa changamoto jeshi la Israeli. Kila siku alipaza sauti hivi: “Chagueni mmoja wa watu wenu ili kupigana nami.” *Eleza kimo cha Goliathi na silaha zake.* ***(1 Samweli 17: 4b-7)*** Mfalme Sauli na jeshi lake waliogopa sana. Hakuna aliyethubutu kupigana na Goliathi. ***(1 Samweli 17: 1-11)*** *Unafikiri askari hao wangefanya nini?*<br>• Kaka watatu wakubwa zake Daudi walikuwa wakipigana katika jeshi la Israeli. *Rudia majina yao, na jinsi ambavyo kati ya hawa wana watatu wakubwa wa Yese hakuna aliyekuwa amechaguliwa na Mungu kuwa mfalme anayefuata wa Israeli.* Daudi alipokuwa akingoja kutawazwa kuwa mfalme, alikuwa ameenda tena kuchunga kondoo za baba yake. Siku moja, Yese alimwambia Daudi apeleke chakula **(Onyesha mkate na jibini)** kwa ndugu zake wanaopigana jeshini. Daudi alifika wakati majeshi yalipokuwa yamejipanga kwa ajili ya vita na akamsikia Goliathi akipiga kelele akiomba mtu atoke kupigana naye. Jeshi la Israeli lilikimbia kwa hofu. Mfalme Sauli aliahidi thawabu kubwa kwa mtu ambaye angepigana na Goliathi na kushinda! ***(1 Samweli 17: 12-25)*** *Waombe watoto wafikirie jinsi Daudi alivyohisi kuhusu jambo hilo.*<br>• Daudi alikasirika kwamba Goliathi alikuwa akilidhihaki jeshi la Israeli. Akasema: “Huyu Mfilisti ambaye ni mmataifa ni nani hata alipe changamoto jeshi la Mungu aliye hai?” Daudi alichukizwa kuona kwamba hakuna mtu angeweza kupigana na hili jitu. Alijua Mungu angewapa ushindi na wangeweza kumuua Goliathi. *Eleza majibu ya Eliabu katika* ***mstari wa 28****.* Mfalme Sauli aliposikia kile ambacho Daudi alisema, alituma watu aitwe. ***(1 Samweli 17: 26-31)***<br>• *Mungu alikuwa ameahidi kuwatunza watu wake, Waisraeli, ikiwa wangemtumaini. Wafilisti waliabudu miungu iliyotengenezwa kwa miti na mawe, lakini Daudi alimwamini Mungu aliye hai. Alijua Mungu angempa ushindi mtu ambaye angejitokeza kwenda kupigana na Goliathi. Ikiwa tunampenda Mungu aliye hai, basi yuko upande wetu, akitutunza.*<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho C – Kukabilina na changamoto (Kupigana na Goliathi). |
| **JIFUNZE** | Fundisha na ueleze Mstari Muhimu – ***1 Samweli 17: 26***. Zingatia sehemu ya mwisho ya mstari. Eleza kuwa wamataifa walikuwa watu wasio Wayahudi ambao waliabudu miungu iliyofanywa na wanadamu, si Mungu aliye hai. |
| **KUMBUKA** | Waombe watoto wachore picha za silaha za Goliathi kwenye safu ya karatasi iliyotumika katika utangulizi na kuandika changamoto yake kwa jeshi la Israeli. Au tumia maswali kwa ajili ya jaribio:<br>• Ni jeshi gani lilikuwa likipigana na Mfalme Sauli na Waisraeli?<br>• Askari wao shujaa aliitwa nani?<br>• Alikuwa na urefu gani?<br>• Taja vipande vya silaha alivyokuwa navyo.<br>• Changamoto yake kwa jeshi la Israeli ilikuwa nini?<br>• Daudi alikuwa akifanya nini ndugu zake walipokuwa jeshini?<br>• Baba yake alimtuma kufanya kazi gani?<br>• Daudi alisikia nini alipofika kwenye kambi ya jeshi?<br>• Ni nini kilimkasirisha Daudi?<br>• Ni nani alituma watu ili kumwita Daudi? |

## C6 Habari ya Tatu
**Daudi – Habari hii inahusu Daudi kumshinda Goliathi.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Mungu alimpa Daudi ujasiri na ushindi dhidi ya Goliathi.<br>• Mungu huwapa ushindi wale wanaompenda na kumwamini.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***1 Samweli 17: 47***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***1 Samweli 17: 32-51*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Rudia C6, habari ya 2, kutoka kwenye vielelezo vya FBI.<br>Waulize watoto kuhusu mambo ambayo yanawatisha. Daudi hakuogopa kupigana na Goliathi kwa sababu alijua Mungu alikuwa pamoja naye. |
| **FUNDISHA** | • Daudi alisimama mbele ya Mfalme Sauli. Simulia mazungumzo katika ***mistari ya 32-33***. Daudi alijua hakuna haja ya kumwogopa Goliathi kwa sababu Mungu alikuwa upande wa jeshi la Israeli. Sauli alifikiri kwamba Daudi alikuwa mdogo sana na hajawahi kupigana kama mwanajeshi. Lakini Daudi alizoea hatari. Alipokuwa akichunga kondoo za baba yake, alikuwa amefanikiwa kupigana na simba na dubu kwa msaada wa Mungu. Haijalishi wewe ni kijana, Mungu anaweza kukusaidia kufanya mambo muhimu. *Simulia kile Daudi anachosema katika **mistari 34-37**.* Daudi alikuwa na uhakika kwamba Mungu angemuokoa asiuawe na Goliathi. ***(1 Samweli 17: 32-37)***<br>• Mfalme Sauli alikubali kwamba Daudi aende kupigana na Goliathi. *Wafanye watoto wafikirie Daudi akijaribu kuvaa silaha za Sauli na anashindwa kutembea kwa sababu ya uzito wake.* Daudi alimwambia mfalme kwamba hangeweza kupigana kwa kuvaa silaha hizo, hivyo akazivua. *Eleza alichofanya katika* **mstari wa 40**. *Onyesha mawe matano laini kwenye mfuko.* ***(1 Samweli 17: 38-40)***<br>• *Eleza jinsi Goliathi alivyotembea kumwelekea Daudi na kumcheka mvulana huyo mchanga asiye na silaha yoyote bali amebeba kombeo tu.* Daudi hakuogopa. Alijua Mungu alikuwa pamoja naye. Alimwambia Goliathi hivi: “Ninakuja kupigana nawe kwa jina la Bwana wa majeshi, Mungu wa majeshi ya Israeli.” *Rejea jinsi ambavyo Wafilisti hawakuabudu Mungu aliye hai, bali miungu ya mawe na miti. Fanya muhtasari wa kile Daudi anachosema katika **mistari 46-47***. Daudi aliweka wazi kwamba hatamshinda Goliathi kwa uwezo wake, bali kwa uwezo wa Mungu. Alijua Mungu alikuwa upande wake. ***(1 Samweli 17: 41-47)***<br>• Mara moja, Daudi aliingiza mkono wake kwenye mfuko wake *(igiza kitendo)*, akatoa jiwe moja na kuliweka kwenye kombeo. Alizungusha kombeo hilo na kupeleka jiwe lile lipae na kuligonga lile jitu katikati ya paji la uso wake **(onyesha)**. Jitu lenye urefu wa mita 3 lilianguka chini. Daudi alitumia **upanga** wa Goliathi kumuua. Jeshi la Wafilisti lilipomwona shujaa wao, Goliathi, amekufa, walikimbia. Mungu alikuwa amempa Daudi na jeshi la Israeli ushindi. *Waongoze watoto washangilie!* ***(1 Samweli 17: 48-51)***<br>• Daudi alimwamini Mungu kwamba angempa ushindi. *Eleza kwamba sio lazima tupigane na majitu. Adui yetu ni Shetani au ibilisi ambaye anataka tufanye mambo mabaya.Tunapaswa kupambana ili tusifanye mambo mabaya katika maisha yetu. Ikiwa tunampenda Mungu na tumemwomba atusamehe dhambi zetu, basi yuko upande wetu. Tukimwomba Mungu, atatusaidia tusifanye mambo mabaya na tuweze kuishi maisha yanayompendeza.*<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho C – Kumshinda Goliathi. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa fundisha na ueleze Mstari Muhimu – ***1 Samweli 17: 47***. *Eleza kuwa maneno haya yalisemwa na Daudi kwa Goliathi.* |
| **KUMBUKA** | • Kwa nini Mfalme Sauli alifikiri kwamba Daudi hakufaa kupigana na Goliathi?<br>• Ni silaha gani za Sauli alizompa Daudi?<br>• Daudi alitumia nini badala yake?<br>• Daudi alimwambia Goliathi nini walipokutana?<br>• Daudi alitumia mawe mangapi kumwangusha Goliathi?<br>• Jeshi la Wafilisti lilifanya nini walipomwona Goliathi amekufa?<br>• Ni nguvu za nani zilimshinda Goliathi?<br>• ‘Adui’ yetu ni nani?<br>• Ni nani atakayetupa ushindi na kutusaidia tusifanye mambo mabaya?<br>Imba wimbo wa "Mvulana Pekee Anayeitwa Daudi" ambao unaweza kupatikana kwenye YouTube. |

<u>C6 Habari ya Nne</u>

**Daudi – Habari hii inahusu kulindwa kwa Daudi.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Wivu ulimfanya Mfalme Sauli amchukie Daudi.<br>• Mungu alimlinda Daudi asidhuriwe na Mfalme Sauli.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***1 Samweli 18: 14***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***1 Samweli 18: 1-16*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Waulize watoto wataje mifano ya wivu. Pendekeza kwamba unaweza kuwa na wivu kwa kile ambacho mtu mwingine anaweza kukifanya - kwa mfano, mtu ambaye ni mwerevu sana au mwanamichezo. Au unaweza kumuonea mtu wivu kama ana kitu ambacho ungependa kiwe cha kwako - kwa mfano, nguo nzuri. Biblia inatufundisha kwamba wivu ni mbaya na unaweza kutusababisha tufanye mambo mabaya ikiwa tutauruhusu ukue. Mungu ametufanya sote kuwa tofauti na tunatakiwa kushukuru kwa kile tulichopewa badala ya kuwaonea wivu wengine. (soma kuhusu wivu katika C1 Habari ya 3) |
| **FUNDISHA** | • Daudi alikuwa shujaa! Baada ya kumuua Goliathi, Mfalme Sauli alifurahishwa sana na Daudi kiasi kwamba alienda kuishi na Mfalme Sauli katika jumba lake la kifalme. Daudi na mwana wa mfalme, Yonathani, wakawa marafiki wazuri. Waliweka ahadi ya kuwa marafiki milele. Yonathani alimpa Daudi zawadi **(orodhesha na kuonyesha vazi na mshipi)** ili kuonyesha urafiki wao ulikuwa na nguvu sana. *Zungumza kuhusu marafiki bora wa watoto.* Ni vizuri kuwa na marafiki ambao wanabaki kuwa marafiki hata kama patokee nini.<br>• Daudi akawa mtu muhimu katika jeshi la Mfalme Sauli. Chochote Sauli alichompa kufanya, alikifanya vizuri. Askari wenzake na watu wa Israeli walifurahishwa naye. Baada ya kumuua Goliathi, Daudi na Mfalme Sauli walirudi Yerusalemu. Wanawake walitoka barabarani wakiwa na matari yao **(onyesho, ikiwezekana)** na vinanda. Sema walichoimba walipokuwa wakicheza. ***(1 Samweli 18: 5-7)***<br>• Unadhani nani alikasirika alipoona hilo likitendeka? *(Mfalme Sauli)* Alikuwa na wivu juu ya Daudi, hata akataka kumuua. *Hasira na wivu husababisha watu kufikiri na kufanya mambo mabaya. Mungu ametuonya kuhusu kuwaonea wivu watu wengine.* ***(Kutoka 20: 17)*** Mfalme Sauli alitafuta nafasi ya kumuua Daudi. Kila siku, Daudi alipiga kinubi chake katika jumba la kifalme na kwa kawaida muziki huo ungemfanya Mfalme Sauli awe mtulivu na asikasirike. Lakini eleza kilichotokea siku iliyofuata alipojaribu mara mbili kumuua Daudi. Sauli alimwogopa Daudi kwa sababu aliona kwamba Mungu alikuwa akimtunza. Aliona kila kitu kinakwenda vizuri kwa Daudi lakini si kwa ajili yake mwenyewe. ***(1 Samweli 18: 8-12)***<br>• Mfalme Sauli alimtuma Daudi kwenda vitani akiwa msimamizi wa watu 1,000. Alifikiri kwamba Daudi angeuawa katika vita. *(Soma* ***1 Samweli 18: 17b****)* Lakini Mungu alimtunza Daudi na Mungu akampa mafanikio katika kila jambo alilofanya. Mfalme Sauli alizidi kuwa na wivu na woga. Lakini watu walimpenda Daudi kwa sababu alikuwa kiongozi wa jeshi mwenye mafanikio. ***(1 Samweli 18: 13-16)***<br>• Daudi alimpenda Mungu, na Mungu alimlinda asipate madhara. Siku moja angekuwa mfalme anayefuata wa Israeli. *Ikiwa tunampenda Mungu na kutafuta kutii yale anayosema katika Biblia, ndipo Mungu atatutunza pia.*<br><br>**Kamilisha Somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho C – Kulindwa. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa fundisha na ueleze Mstari Muhimu – ***1 Samweli 18: 14***. |
| **KUMBUKA** | Andaa vitu vyote ulivyotumia kufundisha C6 (mdoli wa kondoo, mafuta ya mzeituni, mkate na jibini, mawe matano kwenye mfuko, mdoli wa upanga, vazi, mkanda, tari.) Rejelea kwa nini viko kwenye habari, kisha angalia kama watoto wanaweza kuviweka kwa mpangilio sahihi.<br>Watoto wa Daraja la 1 wangefurahia kucheza Mchezo wa Kim – Viweke na kisha ondoa kimoja wakati hakuna anayeangalia. Je, wanaweza kubaini ni kipi kinakosekana? |

# Maelekezo ya waalimu wanaposahihisha masomo

**MASOMO YA DARAJA LA KWANZA:**

- Kurasa nne kwenye kijitabu kina sehemu za kupaka rangi, kujaza maneno machache au kufanya kazi rahisi kila wiki.
- Alama 20 zimewekwa kwa kila wiki na alama 80 kwa kila mwezi.
- Watoto wanaotumia masomo ya Daraja la kwanza hawatarajiwi kuwa wanajua kusoma vizuri. Hivyo basi, tunatarajia wazazi/ walezi/ viongozi wa madarasa kuwasaidia.

**MASOMO YA DARAJA LA PILI:**

- Kurasa 4 kila wiki kwenye vijitabu.
- Habari ya Biblia ipo kwenye somo. Watoto/ wanafunzi wanapaswa kupata baadhi ya maneno kwenye somo, kupaka rangi, kukamilisha Mstari Muhimu na kadhalika.
- Alama 20 zimewekwa kwa kila wiki na alama 80 kila mwezi masomo yanapokamilishwa kwa usahihi.

**KUSAHIHISHA MASOMO YA WAKATI NA BIBLIA**

**VITU VYA KUTUSAIDIA TUNAPOSAHIHISHA**

Waalimu wanaombwa kwanza:

- Kuangalia kila somo na kusahihisha ipasavyo.
- Toa alama kama ulivyoelekezwa.
- Kila mara, tumia wino wa rangi tofauti kusahihisha na kuweka ALAMA YA VEMA (✔) kwenye jibu sahihi.
- Weka au andika jibu sahihi panapostahili na rekebisha makosa yoyote ya maandishi (spelling errors), lakini hakuna alama zinazoondolewa kwa ajili ya kosa hili.
- Toa alama nusu kwa kila jibu ambalo sio sahihi kabisa.
- Jumlisha alama za mwezi na uziandike kwenye nafasi uliyopewa kwa ajili hiyo.

Ni muhimu kuwa mkarimu kama uwezavyo ili kuwatia moyo watoto/ wanafunzi wafanye masomo ya Biblia. Kila mwezi, ni muhimu kwa mwalimu kuandika maneno ya kutia moyo kwenye nafasi iliyowekwa kwa kila mtoto anayemfundisha. Unaweza kuandika kuhusu kupaka rangi vizuri, kufanya kazi safi, alama alizopata mtoto, uelewa wa masomo wa mtoto na kadhalika.

Tunajaribu kutoa mawazo tofauti kama iwezekanavyo. Maswali, maoni, maneno ya kutia moyo na kadhalika, yote yanaweza kutumiwa kuleta utofauti. Kama maoni au usemi mmoja unatumika kila mwezi, watoto watauona hauna maana tena.

**DARAJA LA KWANZA**

**Maoni ya jumla**

"Neema – Ninafurahi kuwa umeanza masomo haya na natumai unayafurahia. Nimependa sana ulivyopaka rangi.
"Je, huwa unaenda shule? Niambie kuhusu shule yako. Ninatarajia kusikia kutoka kwako siku za karibuni."
"Hongera sana Pendo! Umepaka rangi kwa ustadi kweli! Je, ilikuwa vigumu kupaka rangi ndani ya picha tu? Ulikosea kidogo ulipokuwa unapaka rangi kwenye baadhi ya sehemu za somo la mwisho."

**Maoni ya Kiroho**

"Umefanya vyema sana Faraja! Jairo alikuwa na furaha kubwa Yesu alipomsaidia."
"Jibu zuri sana! Habari ya kifo cha Yesu inahuzunisha lakini cha kufurahisha ni kwamba, alifufuka tena."

**DARAJA LA PILI**

**Maoni ya jumla**

"Jibu zuri sana Wema!– "Ninauhakika kuwa, walimu wako wanafurahia sana kazi zako huko shuleni!"
"Debora, naona kuwa tutasherehekea siku yako ya kuzaliwa hivi karibuni. Je, una maandalizi yoyote ya siku hiyo? Je, ni maadalizi gani? Uwe na siku njema!"
"Umejitahidi kweli. Lakini kuna makosa madogo. Usisahau kuhakiki majibu yako kila mara. Mtoto mzuri!"

**Maoni ya Kiroho**

"Napenda ulivyompaka rangi Mtoto Yesu akiwa horini. Je, si inapendeza sana Mungu kumtuma Yesu ulimwenguni kwa ajili yetu?"
"Napenda sana rangi ulizozitumia! Ilimbidi Zakaria kulipa gharama ya kutoamini maneno ya Mungu. Hakukosa kuamini maneno ya Mungu tena."
"Majibu mwafaka kweli! Mtu aliyekutana na Filipo kule jangwani alienda akiwa na furaha kweli. Alisikia na kuamini Habari Njema za Yesu."

## Kiambatisho A – Daraja la Sifuri & la Kwanza Picha kutoka Free Bible Images (FBI)

| | Kichwa cha Habari | Picha za Habari |
|---|---|---|
| C1 | Danieli | **Danieli – Nchi ya ugenini** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/bpa-daniel/ (slides 1 & 2) |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/rg-daniel/ |
| | | **Sanamu ya Nebukadneza na tanuru ya moto** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/fiery-furnace-preschool/ |
| | | **Danieli – Dirisha lililofunguliwa** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/daniel-lions-preschool/ |
| | | **Danieli – Tundu la simba** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/bpa-daniel/ |
| | | |
| C2 | Miujiza Zaidi | **Kipofu aona** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/lgr-blind-man/ |
| | | **Umati walishwa** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/preschool-jesus-5000/ |
| | | **Kiwete atembea** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/yo-jesus-bethesda/ |
| | | **Msichana aliyekufa afufuka** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/preschool-jairus/ |

## Kiambatisho A – Daraja la Pili Picha kutoka Free Bible Images (FBI)

| | Kichwa cha Habari | Picha za Habari |
|---|---|---|
| C1 | Danieli | **Danieli – Nchi ya ugenini** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/daniel-food/ |
| | | **Sanamu ya Nebukadneza na tanuru ya moto** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/meshach-shadrach-abednego/ |
| | | **Danieli – Madirisha yaliyofunguliwa** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/bpa-daniel/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/yo-daniel/ |
| | | **Danieli – Katika tundu la simba** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/yo-daniel/ |
| | | |
| C2 | Miujiza Zaidi | **Kipofu aona** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jesus-blind-man/ |
| | | **Umati walishwa** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/lgr-boy-lunch/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/yo-feeding-5000/ |
| | | **Kiwete atembea** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/yo-jesus-bethesda/ |
| | | **Msichana aliyekufa afufuka** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/lgr-jairus/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jairus-daughter/ |

| Kiambatisho B – Daraja la Sifuri & la Kwanza Picha kutoka Free Bible Images (FBI) | | |
|---|---|---|
| | Kichwa cha Habari | Picha za Habari |
| C3 | Watu aliokutana nao Yesu | **Zakayo** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jesus-zacchaeus-preschool/ |
| | | **Nikodemo** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/rg-nicodemus/ |
| | | **Mwanamke kutoka Samaria** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-018-samaritan-woman/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-019-living-water/ |
| | | **Kijana tajiri** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-074-rich-ruler/ |
| | | |
| C4 | Kifo cha Kristo | **Habari ya Pasaka – Kusalitiwa na Yuda** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/lgr-jesus-passover-1/ |
| | | **Habari ya Pasaka – Pilato** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/preschool-jesus-trial/ |
| | | **Habari ya Pasaka – Yusufu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/preschool-jesus-dies/ |
| | | **Habari ya Pasaka – Wasafiri wawili** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ls-emmaus/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/preschool-jesus-alive/ |

| Kiambatisho B – Daraja la Pili Picha kutoka Free Bible Images (FBI) | | |
|---|---|---|
| | Kichwa cha Habari | Picha za Habari |
| C3 | Watu aliokutana nao Yesu | **Zakayo** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/lgr-zacchaeus/ |
| | | **Nikodemo** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-017-nicodemus/ |
| | | **Mwanamke kutoka Samaria** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jesus-samaritan-woman/ |
| | | **Kijana tajiri** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jesus-rich-man/ |
| | | |
| C4 | Kifo cha Kristo | **Habari ya Pasaka - Yuda** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-085-judas-betrays/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-089-prayer-garden/ |
| | | **Habari ya Pasaka - Pilato** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-092-jesus-pilate/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-093-mocking-jesus/ |
| | | **Habari ya Pasaka - Yusufu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-099-jesus-burial/ |
| | | **Habari ya Pasaka - Wasafiri wawili** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-103-appearance-emmaus/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/disciples-emmaus/ |

## Kiambatisho C – Daraja la Sifuri & la Kwanza Picha kutoka Free Bible Images (FBI)

| | Kichwa cha Habari | Picha za Habari |
|---|---|---|
| C5 | Ruthu & Samweli | **Ruthu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ruth-1/ |
| | | **Ruthu na Boazi** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ruth-1/ |
| | | **Hana amwomba Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ruth-2/ |
| | | **Mungu amwita Samweli** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ruth-3/ |
| | | |
| C6 | Daudi | **Kuchagua mfalme** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/bpa-david/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/fn-samuel-david/ |
| | | **Kupigana na Goliathi** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/bpa-david/ |
| | | **Kumshinda Goliathi** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/bpa-david/ |
| | | **Kuishi na Sauli** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ls-david-saul/ |

## Kiambatisho C – Daraja la Pili Picha kutoka Free Bible Images (FBI)

| | Kichwa cha Habari | Picha za Habari |
|---|---|---|
| C5 | Ruthu & Samweli | **Ruthu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ruth-1/ |
| | | **Ruthu na Boazi** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ruth-2/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ruth-3/ |
| | | **Hana amwomba Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/yo-samuel-saul/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/samuel-born/ |
| | | **Samweli asikia wito wa Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ruth-3/ |
| | | |
| C6 | Daudi | **Kuchagua Mfalme** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/yo-david-goliath/ |
| | | **Kupigana na Goliathi** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/yo-david-goliath/ |
| | | **Kumshinda Goliathi** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/yo-david-goliath/ |
| | | **Kuishi na Sauli** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/david-jonathan/ |

© Bible Educational Services 2020

www.besweb.com

Registered Charity UK CIO 1186004

Swahili - 12/2023